# MWONGOZO

## WA MADEREVA

WA VERMONT




**2024**

**Phil Scott**, Gavana wa
Jimbo la Vermont

**Joe Flynn**, Katibu wa Shirika
la Usafiri

**Wanda Minoli**, Kamishna wa
Idara ya Magari

VERMONT

**Kuangalia NDIYO**
**Inaweza Kuokoa Maisha**




# Ufadhilii wa Kiungo cha Mwili Huokoa Maisha

Unapoomba leseni yako, utakuwa na fursa ya kuwa mfadhili aliyesajiliwa.

## Kusema 'Ndiyo' kunaweza kuokoa maisha!

**Ukweli:** Kusema "Ndiyo" kwa ufadhili hakutaathiri huduma yako ya matibabu.
**Ukweli:** Hakuna gharama kwa mfadhili au familia yake kwa ufadhili kufanyika.
**Ukweli:** Dini zote kuu huunga mkono ufadhili wa kiungo cha mwili na tishu au huona hilo kama uamuzi wa mtu binafsi.
**Ukweli:** Nchini Marekani, ni kinyume cha sheria kununua au kuuza viungo na tishu kwa ajili ya uhamishaji.

**Una uwezo wa kufadhili maisha!**

Kwa habari zaidi tembelea DonateLifeVT.org

VERMONT IDARA YA MAGARI
IDARA YA AFYA

Somea mtihani wako wa Kibali cha Mwanafunzi na ujifunze kuendesha kwa salama kwa kutumia mafunzo yetuya mtandaoni,




DriveVermont. Unaweza kutumia DriveVermont kujifunza sheria za barabarani na jinsi ya kuendesha gari kwa usalama unaposomea mtihani wako wa Kibali cha Mwanafunzi. Unaweza pia kujua kile unachohitaji kutambua kabla ya kufanya mtihani wako wa maandishi au wa barabarani.

Utapata DriveVermont imejaa picha na video za kufaa. Maswali ya kuhusisha yatakusaidia kujitahini juu ya kile umejifunza. Baada ya kumaliza mafunzo, unaweza kufanya mtihani wa mazoezi ambao utaonekana sawa na mtihani halisi utakaofanya.

Kuanza kusomea kibali chako na kujifunza kuendesha gari kwa salama tembelea dmv.vermont.gov

---

Idara ya Magari haibagui watu wenye ulemavu katika utoaji wa huduma, programu, shughuli au ajira.

Idara ya Magari itaweka fadhila za kufaa wakati ulemavu wa mtu unaingilia kwa kiasi kikubwa uwezo wake wa kuelewa habari inayotolewa kwa kupata Kibali cha Mwanafunzi au Leseni ya Udereva.

Ikiwa, kwa mfano, ulemavu wako unapunguza uwezo wako wa kusoma na kuelewa lugha iliyoandikwa, unaweza kupata sauti au matoleo shirikishi ya mtandaoni ya mwongozo huu ambayo yanapatikana kwenye tovuti yetu. Ikiwa unahisi kuwa Idara ya Magari haijakupa fadhila ya kufaa kwa ulemavu wako, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume ya Haki za Binadamu ya Vermont kwa kupiga simu 800.416.2010.

Ikiwa una tatizika kusoma au una ulemavu unaozuia uwezo wako wa kusoma, tujulishe unapofanya miadi yako. Tutashughulika nawe ili kukidhi mahitaji yako.

Mtihani wa Kibali cha Mwanafunzi haufanywi tena katika ofisi yetu. Ni mtihani wa mtandaoni unaopatikana kwenye tovuti yetu, mydmv.vermont.gov.

VN-007 11/2023 MTC

## Ujumbe wa Usalama kutoka kwa Kamishna



Uamuzi wako wa kupata Kibali cha Mwanafunzi au Leseni ya Dereva una mojawapo ya majukumu makubwa zaidi ya kijamii maishani Unajitolea: kutunza gari linaloendeshwa kwa usalama ambalo linafikia viwango vya uchafuzi wa hewa vya Vermont, kubeba bima ya dhima, daima kutii sheria za barabarani, na kufuata mienendo inayoondoa mivuto ya mawazo wakati wa kuendesha gari.

Kugongana kwa magari ndio sababu kuu ya kulazwa hospitalini na vifo kutokana na majeraha. Watu wa umri wote huathirika, iwe ni dereva, abiria, au mtu wa familia ya mwathiriwa wa mojawapo ya ajali hizi.

Kuwa na leseni ni haki ambayo hupatikana kwa kuonyesha ujuzi wako wa kuendesha gari kwa njia ambayo hudhihirisha wewe ni dereva stadi na salama. Kudumisha haki hiyo kunahitaji wewe uendelee kuendesha gari lako kwa njia salama na ya uwajibikaji.

Tutajaribu kuufanya mtihani wako wa kuendesha gari kuwa uzoefu mzuri ingawa tunatambua wasiwasi unaohusishwa na kutahiniwa.

Kumbuka kuwa unatumia barabara kuu na kila mtu mwingine. EPUKA MIVUTO YA MAWAZO NA UENDESHA GARI KWA SALAMA.



Wanda Minoli Kamishna

Mwongozo huu umetengenezwa na Idara ya Magari ya Vermont na kupigiwa chapa Vermont. Tafadhali saidia kupunguza gharama kwa serikali ya jimbo kwa kurejesha mwongozo huu au kumpa dereva mwingine wa baadaye.

MWONGOZO HUU HAUWEZI KUTUMIWA WAKATI WA JARIBIO

# Yaliyomo

Sura ya 1 - Habari ya Jumla ........ 5
Sura ya 2 - Jinsi ya Kupoteza Leseni Yako ........ 7
Sura ya 3 – Thibitisho la Utambulisho ........ 8
Sura ya 4 – Taarifa ya Leseni ya Jumla ........ 12
Maswali na Majibu Kuhusu Kibali cha Mwanafunzi ........ 12
Maswali na Majibu Kuhusu Leseni za Udereva wa Vijana ........ 13
Maswali na Majibu Kuhusu Leseni za Dereva ........ 16
Sura ya 5 - Mpango wa Leseni ya Dereva ya Hatua kwa Hatua ........ 20
Sura ya 6 – Ada, Kupata leseni tena na Kubadilisha ........ 23
Sura ya 7 - Kuendesha Gari kwa Usalama na Kusomea Kibali Chako ........ 25
Jinsi ya Kuendesha Gari kwa Usalama ........ 25
Kuegesha Gari Lako ........ 29
Mizunguko ........ 29
Vizuizi vya Polisi ........ 30
Sheria ya Kusogea ........ 31
Taa za Trafiki, Ishara za Barabara, na Alama za Barabara Kuu ........ 31
Ishara za Barabara ........ 32
Kutumia Barabara moja ........ 37
Hali ya Uendeshaji Hatari ........ 46
Kuendesha Gari Kwenye Barabara kuu za Jimbo ........ 50
Kuendesha Gari Ukiwa Umeathirika ........ 52
Kuendesha Gari Ukiwa na Mvuto wa Mawazo ........ 54
Mtihani wa (Ujuzi) Barabara ........ 56
Sura ya 8 - Mfumo wa Pointi ........ 64
Sura ya 9 – Umiliki wa Gari ........ 65
Sura ya 10 – Leseni ya Dereva ya Biashara ........ 70
Sura ya 11 - Watu wenye Ulemavu ........ 71
Sura ya 12 – Wazazi au Walezi ........ 73

### SIKUKUU ZA JIMBO LA VERMONT

| | |
|---|---|
| Sikukuu ya Mwaka Mpya | Januari 1 |
| Siku ya Martin Luther King, Jr. | Jumatatu ya 3 Januari Siku |
| ya Marais | Jumatatu ya 3 ya Februari |
| Siku ya Mkutano wa Mji | Jumanne 1 ya Machi |
| Siku ya Kumbukumbu | Jumatatu ya Mwisho ya Mei |
| Sikukuu ya Uhuru | Julai 4 |
| Sikukuu ya Vita vya Bennington | Agosti 16 |
| Sikukuu ya Wafanyakazi | Septemba 1 Jumatatu |
| Sikukuu ya Mashujaa | Novemba 11 |
| Sikukuu ya Shukrani | Alhamisi ya 4 Novemba |
| Siku Baada ya Sikukuu ya Shukrani | Ijumaa baada ya Shukrani |
| Sikukuu ya Krismasi | Desemba 25 |

Ofisi zote hufungwa tarehe zilizo hapo juu, na tarehe zilizoadhimishwa kama ilivyoelezwa hapa chini.

Sikukuu inayoangukia Jumamosi itaadhimishwa Ijumaa inayotangulia. Sikukuu inayoangukia Jumapili itaadhimishwa Jumatatu inayofuata.

Mtahini huenda asiwepo kila wakati kwa sababu ya mtihani wa barabarani. Tafadhali kuwa na subira. Mtahini atakusaidia haraka iwezekanavyo.

Wakati mwingine inaweza kuwa muhimu kufuta au kuahirisha mtihani wa udereva kwa sababu ya hali mbaya ya barabara. Piga simu 802.828.2000 au tembelea mydmv.vermont.gov ili kupanga upya, ikiwa ni lazima.

**Imeandaliwa na:**

VERMONT

**Idara ya Magari**
120 State Street
Montpelier, Vermont 05603-0001
**dmv.vermont.gov**



**MAENEO YA OFISI**

### Bennington
Bennington County
530 Main St

### Dummerston
Windham County
AOT District #2 Office,
Route 5

### Montpelier
Washington County - **Ofisi Kuu**
120 State Street

### Newport
Orleans County
100 Main Street

### Saint Albans
Franklin County 27
Fisher Pond Rd

### Saint Johnsbury
Caledonia County Green
Mtn Mall,
1998 Memorial Dr

### South Burlington
Chittenden County 4
Market Street

### Springfield
Windsor County
100 Mineral St, Suite 103

### Rutland
Rutland County
101 State Place

### White River Junction
Windsor County 221
Beswick Drive

Ziara zote za ofisi ni kwa miadi tu. Ili kupanga miadi, tembelea mydmv.vermont.gov au piga simu 888.970.0357

**Mawasiliano**
dmv.vermont.gov/contact
facebook.com/VermontDMV
**802.828.2000**
**888 99-VERMONT (888-998-3766)**
Walio na Shida ya Kusikia Piga 711

**Unawezaje kupoteza leseni yako au Haki ya Kuendesha Gari?**

**7 V.S.A. § 656 - Watoto kudanganya umri wao, kununua, kumiliki, au kunywa pombe; kosa la kwanza; ukiukaji wa haki za kiraia**

Ukikamatwa na kuandikiwa shtaka, utahitajika kuwasiliana na Programu ya Usalama wa Pombe kwa Vijana (TASP) ya Mchepuo wa Mahakama ya Vermont (kushindwa kuwasiliana na bodi ya mchepuo ndani ya siku 15 kutasababisha kesi hiyo kupelekwa kwa ofisi ya mahakama, ambapo mtu, ikiwa atapatikana na hatia ya ukiukaji, atakabiliwa na adhabu ya $300.00 na Leseni yake ya Udereva kusimamishwa kwa siku 90, na anaweza kukabiliwa na ongezeko kubwa la viwango vya bima) na kushiriki katika tathmini ya matumizi mabaya ya pombe, kufuata mapendekezo ya mshauri na mahitaji mengine. Programu hizi zote zinahitaji ada ya ziada. Aidha ukikosa kukamilisha TASP au mahitaji mengine ya Mchepuo, leseni yako au haki ya kuendesha gari ITASIMAMISHWA. Ada za ziada zitastahili kulipwa kwa DMV ili irejeshwe.

**23 V.S.A. § 202 - Kuiga Mtu Mwingine Katika Ombi, Au Kusaidia Muombaji Kwa Uwakilishi wa Uongo**

Mtu anayeiga mwingine kwa uwongo katika maombi ya Leseni ya Udereva au Kibali cha Mwanafunzi, au katika maombi ya kitambulisho kisicho cha dereva, au katika maombi ya usajili wa gari, gari la matumizi ya ardhi zote, usajili wa kigari cha theluji au boti, au uhalalishaji wa chombo, au anayepata leseni ya kuendesha gari kwa njia ya uwongo, au anayepata Kibali cha Mwanafunzi au kadi ya kitambulisho kisicho cha dereva kwa njia ya uwongo, au anayepata usajili wa gari au usajili wa aina nyingine yoyote ya gari au chombo kwa njia ya uwongo, au ambaye anatumia jina bandia au jina lisilo lake mwenyewe katika maombi ya Leseni ya Udereva, au Kibali cha Mwanafunzi au katika maombi ya kitambulisho kisicho cha dereva, au katika maombi ya usajili wa gari, au usajili kwa gari au chombo kingine chochote, au ambaye kwa kimakusudi anamsaidia mwombaji kupata leseni, kibali, usajili au kadi ya kitambulisho kisicho cha dereva kwa njia ya uwongo wa umri au utambulisho wa mwombaji huyo, atatozwa faini isiyozidi $1,000 au kifungo kisichozidi miaka miwili, au vyote viwili na haki yake ya kuendesha gari itasimamishwa kwa siku 90.

**MFUMO WA KUASHIRIA MADEREVA WAVUNJA SHERIA**

Baada ya kutuma maombi ya Kibali cha Mwanafunzi, Leseni ya Udereva wa Vijana au Leseni ya Dereva, uchunguzi utafanywa kwenye Mfumo wa Kitaifa wa Kuashiria Madereva Wavunja Sheria (PDPS). Ikiwa matokeo ya uchunguzi wa PDPS yataonyesha kuwa umesimamishwa, umebatilishwa, umekataliwa, au kughairiwa katika jimbo jingine, ombi lako la Leseni ya Dereva ya Vermont , Leseni ya Mwanafunzi au Leseni ya Dereva Kijana litakataliwa hadi wakati tutakapopokea thibitisho kuwa umerejeshewa leseni au kuondolewa makosa katika jimbo hilo. Ikiwa umesimamishwa, kubatilishwa, kunyimwa, au kughairiwa katika jimbo jingine, huenda usitahiniwe au kupata Leseni ya Dereva.

# Sura ya 3 – Thibitisho la Utambulisho

Utahitaji hati kutoka kwa **kila moja ya makundi 4** hapa chini:

1. Utambulisho na Tarehe ya Kuzaliwa
2. Taarifa ya Usalama wa Jamii
3. Makazi ya Vermont na Anwani ya Sasa
4. Hali Yako ya kisheria nchini Marekani (Inahitajika tu kwa hati ya Real ID na leseni ya EDL)

Kumbuka:
- Hati ni lazima ziwe za asili, au nakala zilizothibitishwa na shirika linalotoa. Hati za kutumwa na faksi au za kunakiliwa HAZITAKUBALIWA.
- Hati zinaweza kufanyiwa ukaguzi na idhinisho la idara. Maelezo ya ziada yanaweza kuhitajika.
- Katika hali zingine, idhinisho la hati huenda lisifanyike siku hiyo hiyo na linaweza kuhitaji ziara ya ziada.
- Hati za asili zinazotolewa kwa DMV zitarejeshwa kwa mwombaji na zinaweza kupigwa picha na kuhifadhiwa kwenye hifadhidata salama.
- Ikiwa jina lako ni tofauti na lile lililoandikwa kwenye hati zako, lazima utoe thibitisho la mabadiliko ya kisheria (cheti cha ndoa, amri ya talaka, amri ya korti, nk.)

## Utambulisho na tarehe ya kuzaliwa:

Lazima utoe moja ya zifuatazo:

- Pasipoti halali, ambayo muda wake haujaisha
- Rekodi iliyothibitishwa ya kuzaliwa kwa mwombaji, ndoa, kupangwa utotoni, au talaka, ikiwa pamoja na tafsiri kama ni lazima
- Ripoti ya Ubalozi ya Kuzaliwa Nje ya Nchi (CRBA) iliyotolewa na Marekani Idara ya Jimbo (Form FS-240, DS-1350 or FS-545)
- Hati halali ya utambulisho wa ubalozi iliyotolewa na serikali ya Meksiko, Guatemala (au serikali nyingine yoyote iliyo na viwango vya usalama na itifaki zinazolingana, kama ilivyoamuliwa na Kamishna)
- Kadi Halali ya Makazi ya Kudumu ambayo Tarehe haijafika mwisho (Form I-551)
- Cheti cha Kuandikisha Uraia kilichotolewa na DHS (Form N-550 au Form N-570)
- Cheti cha Uraia (Form N-560 au Form N-561) kilichotolewa na DHS
- Leseni ya Dereva ya Real ID au Kitambulisho kilichotolewa kwa kufuata viwango vilivyowekwa na 6 CFR part 37
- Kama jina lililopo kwenye leseni ni/litakuwa tofauti na jina linaloonekana kwenye hati ya msingi (kwa mfano, kupitia ndoa, kupangwa utotoni, amri ya mahakama, au utaratibu mwingine unaoruhusiwa na sheria ya Jimbo au kanuni), ushahidi wa mabadiliko ya jina kupitia uwasilishaji wa hati zilizotolewa na mahakama, shirika la serikali au chombo kingine kama ilivyoamuliwa na Kamishna unahitajika. DMV itabaki na nakala za hati zilizowasilishwa na kuhifadhi rekodi ya jina lililorekodiwa na jina lililo kwenye hati za msingi za asili.

Kumbuka: hati za ziada zinaweza kuhitajika kwa hiari ya Idara ya Magari ikiwa hati iliyowasilishwa inatiliwa shaka au kama kuna sababu ya kuamini mtu huyo sio yule anayedai kuwa. Wafanyakazi wa leseni ya dereva wataamua kama hati

zilizotolewa kutoka kwenye orodha hii ni halisi, halali, na za kukubalika. Hati zilizonakiliwa na kutumwa kwa faksi HAZITAKUBALIWA.

**Leseni ya Dereva Iliyoboreshwa (EDL) inahitaji Thibitisho la uraia wa Marekani:**

Raia wa Marekani wanaorejea kutoka Kanada, Meksiko, Karibea, au Bamuda, kwa nchi kavu au bahari, wanatakiwa kuwasilisha Pasipoti ya Marekani, Kadi ya Pasipoti ya Marekani au Leseni ya Dereva Iliyoboreshwa (EDL). EDL inahitaji thibitisho la Uraia wa Marekani pamoja na thibitisho la utambulisho, SSN na Ukaaji wa Vermont.

## Taarifa ya Usalama wa Jamii

Lazima uwasilishe kadi yako ya Usalama wa Jamii au barua kutoka kwa Mamlaka ya Usalama wa Jamii inayoonyesha kutostahili kupokea nambari ya Usalama wa Jamii (SSN).

Ikiwa kadi yako ya Usalama wa Jamii haipatikani, mojawapo ya fomu zifuatazo inaweza kutumika mahali pake:

- Fomu ya W-2,
- Fomu ya SSA-1099,
- hati ya mshahara ikionyesha jina na SSN (kiasi cha tarakimu 4 za mwisho)

### Taarifa iliyosahihishwa / Mabadiliko ya Jina

Jina lako lazima lithibitishwe na Mamlaka ya Usalama wa Jamii. kama unahitaji kurekebisha au kusasisha habari katika Mamlaka ya Usalama wa Jamii, fanya hivyo kabla ya kutembelea DMV. Lazima uje na kadi yako ya Usalama wa Jamii iliyosasishwa unapoomba Leseni ya Dereva iliyorekebishwa au kadi ya kitambulisho ya jina lako jipya. Kwa habari kuhusu jinsi ya kufanya hivyo, tembelea socialsecurity.gov.

### Kubadilisha Kadi ya Usalama wa Jamii

Mamlaka ya Usalama wa Jamii hutoa huduma za mtandaoni kwa wakazi wa Vermont inayopatikana kupitia kwa tovuti ya Usalama wa Jamii mtandaoni. Hili huruhusu watu kuomba upya kadi yao ya SSN kutoka nyumbani mwao au ofisi, bila hitaji la kusafiri hadi ofisi ya Usalama wa Jamii. Kwa habari kuhusu jinsi ya kufanya hivyo, tembelea socialsecurity.gov.

### Raia wa Kigeni

Ikiwa wewe ni raia wa kigeni wa muda ambaye hajaidhinishwa kuajiriwa, unahitajika kuwasilisha barua kutoka kwa Mamlaka ya Usalama wa Jamii kuthibitisha huna SSN. DMV ya Vermont itathibitisha nambari yako ya USCIS. DMV ya Vermont haitatoa Leseni ya Dereva au Kitambulisho kama umebaki na chini ya siku 30 za kuwa Nchini Kihalali. DMV ya Vermont itathibitisha jina lako kielektroniki, tarehe ya kuzaliwa na SSN ikiwa na Mamlaka ya Usalama wa Jamii. Hakikisha hati yako imesasishwa na ni sahihi ili kuepuka kuchelewa.

## Makazi ya Vermont na Anwani ya Sasa

Ili kupata Leseni mpya ya Dereva ya Vermont, Leseni ya Dereva Iliyoboreshwa, Kibali cha Mwanafunzi, Kitambulisho kisicho cha Dereva, au Leseni ya Udereva ya Biashara waombaji lazima watoe thibitisho la makazi ya Vermont. Isitoshe, waombaji walio na anwani ya nje ya makazi watahitajika kuthibitisha makazi ya Vermont wakati wa kuomba upya hati yoyote iliyo hapo juu.

Ile *anwani ya makazi* unayotoa lazima iwe anwani ya mtaa au barabara kuu. Hiwezi kuwa sanduku la posta. Katika maeneo ambayo nambari na jina la mtaa hazijateuliwa rasmi, mkataba wa anwani unaotumiwa na Huduma ya Posta ya Marekani inakubalika. Unaweza kutumia sanduku la posta kama anwani yako ya barua.

Kama barua hupokewa kwenye anwani ya mtaa:

- Barua mbili zikiwa na jina la sasa na anwani ya mtaa.

Kama barua haijapokewa kwenye anwani ya mtaa, toa mbili (2) kati ya zifuatazo zinazoonyesha anwani ya mtaani:

- Bili ya matumizi (lazima iorodheshe anwani ya huduma).
- Bili ya kodi ya mali ikionyesha na eneo kamili.
- Taarifa ya Mkataba wa kukodisha ama ya Mwenye nyumba.
- Kadi ya Vermont ya EBT (Uhamisho wa Manufaa ya Kielektroniki) au kadi ya utambulisho ya Vermont AIM (Usimamizi wa Taarifa Kuu).
- Bima ya Wamiliki Nyumba/Wapangaji (sera/ushahidi wa madai).
- Kama mwombaji anaishi na watu wengine na hapati barua kwenye anwani yake ya mtaa:
- Cheti cha Makazi ya Vermont Kilichokamilishwa na akiwasilishe na maombi.

**Jeshi la Marekani, Ako Jeshini**

- Kama anaishi Vermont, angalia hapo juu.
- Kama anaishi nje ya jimbo, kitambulisho cha kijeshi na thibitisho kuwa Vermont ni makazi yake katika rekodi za kijeshi, kama vile Taarifa ya Likizo na Mshahara au maagizo.

**Watoto**

- Cheti cha Makazi ya Vermont na hati moja (1) ya makazi ya wazazi kutoka hapo juu.
- Ushahidi wa uhusiano wa Mzazi/Mlezi na mwombaji.

**Mahitaji ya Makazi ya Kibali cha Mwanafunzi ya Vermont**

Kuthibitisha makazi ya Vermont, mwombaji lazima atoe kwa Idara mojawapo ya hati zilizoonyeshwa hapo juu. Ikiwa mwombaji ni mtoto, Mzazi/Mlezi atahitajika kutoa mojawapo ya hati za makazi.

Kama mwombaji sio mkazi wa Vermont, anaweza tu kupata Kibali cha Mwanafunzi cha Vermont kwa madhumuni ya kushiriki katika elimu ya dereva na kozi ya mafunzo. Mwombaji lazima ape Idara mojawapo ya zifuatazo:

- Barua kutoka kwa Mshauri wa shule inayosema mwanafunzi/mwombaji anapaswa kujiandikisha katika kozi ya elimu ya udereva, ama

- Barua kutoka kwa Shule ya Kufunza Udereva inayoonyesha mwombaji/mwanafunzi ameandikishwa darasani.

## Hali halali nchini Marekani (Inahitajika kwa Real ID na EDL tu)

Mara nyingi, hati zinazohitajika kwa uthibitisho wa utambulisho na tarehe ya kuzaliwa pia zitazatiti hali halali nchini Marekani. Raia wa kigeni lazima watoe pasipoti na visa, kadi ya stakabadhi ya usajili wa wageni (kadi ya visa ya bahati nasibu), au uthibitisho mwingine wa uwepo wa kisheria kwa ukaguzi na kunakili.

DMV ya Vermont hutumia hutumia programu ya Idara ya Usalama wa Taifa ya Marekani inayojulikana kama unaojulikana kama Uthibitishaji wa Utaratibu wa Kigeni kwa Haki (SAVE) ili kuthibitisha kielektroniki hati za uhamiaji zinazotolewa na Idara ya Usalama wa Taifa ya Marekani au Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani.

- Kama unaomba Leseni Iliyoboreshwa (EDL) thibitisho la Uraia wa Marekani linahitajika.
- Thibitisho la Hali Halali lazima liwe na *angalau siku 30 zilizobaki*.

## Kadi ya Kuendesha gari Kihalali

Kadi ya Kuendesha gari Kihalali ni leseni ya Vermont au kibali ambacho sio ridhaa ya Real ID.

Kadi ya Kuendesha gari Kihalali inapatikana kwa mtu yeyote ambaye ni Mkazi wa Vermont. Utoaji wa DPC hauhitaji thibitisho la uwepo wa kisheria au uraia wa Marekani.

## Viashirio Vilivyotambulishwa vya Kibinafasi

Vifuatavyo ni viashirio vilivyotambulishwa vya kibinafsi vya Leseni ya Dereva ya Vermont ama kadi ya Kitambulisho kisicho cha Dereva.

- Urefu
- Uzito
- Rangi ya macho
- Jinsia

Waombaji hawahitajiki chini ya sheria za Vermont au za serikali kuu kuwasilisha hati zinazothibitisha habari wanayowasilisha kwa maingizo haya.

# Sura ya 4 – Maelezo ya Jumla ya Leseni

**Leseni**

Kama unaishi Vermont na unapanga kuendesha gari huko Vermont, lazima upate leseni ya dereva ya Vermont. Mtu ambaye amehamia jimbo kutoka kwa mamlaka nyingine akiwa na leseni halali kutoka jimbo hilo atapata leseni ya Vermont ndani ya siku 60 za kuhamia Vermont.

Kwa mujibu wa sheria ya jimbo na ya serikali kuu, mtu yeyote aliye na leseni ya dereva ya kibiashara kutoka jimbo jingine lazima aihamishe leseni hiyo ya kibiashara ndani ya siku 30 za kuanzisha makazi huku Vermont.

Tendo la kupata leseni hufanya kuendesha gari kuwe haki, na kuwa na leseni inahitaji uendeshe gari ndani ya mipaka ya sheria na kutendea watumiaji wote wa barabara kuu, ikiwa ni pamoja na waendesha baiskeli, waendesha pikipiki, na watembea kwa miguu kwa heshima na wema.

Ushawishi wako kwa maisha ya wengine utapanuka sana, kama vile jukumu lako unapokalia kiti cha dereva cha gari. Mitihani wa leseni hupima maarifa na ujuzi wako. Ni jukumu lako kuendesha gari kwa usalama na ifaavyo.

**Aina za Leseni**

- Kibali cha Mwanafunzi
- Leseni ya Dereva
- Leseni ya Udereva ya Mtoto
- Leseni ya Dereva ya Kibiashara (CDL)
- Leseni ya Dereva Iliyoboreshwa (EDL)
- Kadi ya Kuendesha gari Kihalali

## Maswali na Majibu kuhusu Kibali cha Mwanafunzi

**Ni nani anayehitaji Kibali cha Mwanafunzi?**

Kama wewe ni mkazi wa Vermont na unataka kuendesha gari huko Vermont, itabidi upate Kibali cha Mwanafunzi cha Vermont. Lazima angalau uwe na umri wa miaka 15 ili kufanya mtihani. Mkazi wa Jimbo lingine aliyejiandikisha katika kozi ya Elimu na Mafunzo ya Dereva ya Vermont pia anaweza kupata Kibali cha Mwanafunzi cha Vermont (Barua kutoka shule inayothibitisha ujiandikishaji itahitajika).

**Je, ninahitaji kufanya nini ili kupata Kibali cha Mwanafunzi?**

1. Kama una umri wa miaka 15, 16 au 17, unahitaji idhini ya mzazi wako au mlezi wa kisheria (isipokuwa uwe ni mtoto wa kujitegemea). Mzazi au mlezi wa kisheria lazima atie saini ombi kabla ya wewe kufanya mtihani. Kama wewe ni mwanafunzi wa kigeni anayesoma kwa muda, unaweza kupata Fomu ya Idhini ya Wazazi ya Wageni Wanaosoma kwa muda (VL-036) ili itiwe saini na mzazi au mlezi wa kisheria. Mzazi mwenyeji hawezi kusaini.
2. Kibali chako kitatolewa baada ya kupita mtihani wa kibali mtandaoni na kulipa ada inayohitajika.

Kuomba Kibali cha Mwanafunzi, mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 lazima awe amedumisha rekodi 'safi' ya kuendesha gari katika miaka miwili (2) iliyopita . Kama umekuwa na kusitishwa kwokwote, kusimamishwa, au kubatilishwa, wasiliana na DMV kwani unaweza kuhitajika kupewa kipindi cha ziada cha kusubiri.

**Ni wakati gani na wapi ninaweza kuendesha gari nikitumia Kibali?**

Ukiwa na Kibali cha Mwanafunzi, unaweza kuendesha gari mahali popote, wakati wowote huko Vermont ikiwa kuna mzazi au mlezi aliye na leseni na asiyedhurika, au mwalimu aliyeidhinishwa au kuthibitishwa wa elimu ya udereva asiyedhurika au mtu aliyeidhinishwa na asiyedhurika, mwenye leseni na umri wa miaka 25 au zaidi akiwa kiti cha mbele. Kabla ya kuendesha gari katika jimbo lingine lolote, lazima uwasiliane na Idara ya Magari ya Jimbo hilo au wakala wa utekelezaji wa sheria ili kuona kama ni halali kuendesha gari katika jimbo hilo ukiwa na Kibali cha Mwanafunzi cha Vermont.

## Maswali na Majibu kuhusu Leseni za Dereva Kijana

**Nani anaweza kupata Leseni ya Dereva Kijana?**

Mtu lazima awe amedumisha rekodi 'safi' ya kuendesha gari bila Kibali chake cha Mwanafunzi kusitishwa wakati wowote, kusimamishwa, au kubatilishwa kwa kipindi cha miezi sita (6) kabla ya kupata Leseni ya Dereva Kijana.

Mtu lazima awe na Kibali cha Mwanafunzi kwa angalau mwaka mmoja (1) kabla ya kupata Leseni ya Dereva Kijana.

Leseni ya Dereva Kijana hutolewa kwa watu wenye umri wa miaka 16 au 17 ambao wanapita mtihani unaohitajika. Mzazi wako au mlezi wa kisheria lazima atie saini ombi lako la kukupa kibali cha kutahiniwa.

Kabla ya kupata leseni, wote wenye umri wa miaka 16 na 17 lazima wawe wamepita elimu ya dereva iliyoidhinishwa na serikali na kozi ya mafunzo yenye saa 30 ya masomo ya darasa, saa 6 za udereva na saa 6 ya uchunguzi wa macho. Mamlaka ya Elimu ya Vermont, Idara ya Elimu ya Udereva, husimamia kozi za elimu ya dereva katika shule za upili. Pia kuna shule za mafunzo ya madereva wa kibiashara za Vermont ambazo hutoa kozi za mafunzo ya dereva. Mbali na masaa yaliyoonyeshwa hapo juu, lazima ukamilishe saa 40 za mazoezi ya kuendesha gari, na angalau saa 10 zikiwa za kuendesha gari usiku. kuendesha gari usiku huchukuliwa kuwa kipindi cha dakika 30 baada ya jua kuzama, hadi dakika 30 kabla ya mapambazuko

**Nahitaji Nini ili kupata Leseni ya Dereva Kijana?**

1. Kibali cha Mwanafunzi wa Vermont ambacho hakijaisha muda wake. Mtu anaweza kufanya jaribio la barabara ikiwa Kibali cha Mwanafunzi hakijapitisha zaidi ya miaka 3 kabla kiishe na kimefanywa upya kabla ya mtihani. Kama kimeisha kwa zaidi ya miaka 3, mtihani wa maandishi utahitajika kabla ya jaribioi la barabara kutolewa.

2. Kukamilisha kwa mafanikio kozi ya elimu ya udereva iliyothibitishwa na Mamlaka ya Elimu ya Vermont au Idara ya Magari ya Vermont. Mwalimu wako lazima awe ameandikisha kamilisho lako katika Huduma ya Vyeti vya Elimu ya Udereva kabla Jaribio la Kuendesha gari kufanyishwa. Elimu ya udereva wa nje ya jimbo inakubalika tu ikiwa kozi hiyo ilifundishwa na mwalimu aliyeidhinishwa na/au mwenye leseni ya elimu ya udereva na inajumuisha mafunzo ya darasa na ya kuendesha gari. Ikiwa cheti cha kukamilisha hakikutolewa na wakala wa serikali, mwombaji lazima awasilishe hati iliyo na karatasi yenye anwani ya jimbo kutoka kwa wakala sahihi inayoonyesha kuwa mpango wa elimu ya udereva unaotambulika ulitoa cheti, na lazima iorodheshe mahitaji ya chini ya kukamilisha programu kwa mafanikio.

3. Mzazi au mlezi wako lazima athibitishe kuwa umekamilisha saa 40 za mazoezi ya kuendesha gari, na angalau saa 10 za kuendesha gari usiku. Unaweza kutumia Karatasi ya Kumbukumbu ya Mazoezi ya Kuendesha gari (fomu VN-219) ama Programu ya RoadReady kufuatilia maendeleo yako. **Kumbuka:** Sheria inahitaji saa 40 za mazoezi ya kuendesha gari pamoja na saa 6 za kuendesha gari kunakohitajika ili kukamilisha kwa mafanikio elimu ya udereva.

4. Unahitaji ruhusa ya mzazi wako au mlezi wa kisheria (isipokuwa uwe mtoto wa kujitegemea). Mzazi au mlezi wa kisheria lazima atie saini ombi kabla ya wewe kufanya mtihani. Kama wewe ni mwanafunzi wa kigeni anayesoma kwa muda, lazima kwanza upate Idhini ya Wazazi ya Wageni Wanaosoma kwa muda (fomu VL-036) ili itiwe saini na mzazi au mlezi wa kisheria. Mzazi wako mwenyeji hawezi kutia saini fomu hii. Fomu hii inapatikana katika ofisi za Idara ya Magari.

5. Lazima uweke Nambari yako ya Usalama wa Jamii kwenye ombi au utoe barua kutoka kwa Mamlaka ya Usalama wa Jamii inayoonyesha kutostahiki kwako kupata Nambari ya Usalama wa Jamii.

6. Panga miadi kwa ajili ya mtihani.

7. Kuwa na gari ambalo ni safi, katika hali nzuri ya mitambo, halali, iliyo na kibandiko thabiti cha ukaguzi. Hakikisha kuwa breki ya dharura/ya kuegesha inafanya kazi vizuri.

8. **Kuwa tayari:** Tafuta kadi halali ya bima kama inavyotakiwa na Sheria ya Vermont na usajili wa gari kabla ya kufika kwa miadi yako. Kukosa kuonyesha kadi halali ya bima na cheti cha usajili kutazuia kutahiniwa. Kadi ya bima lazima ieleze jina la mtoa huduma wa bima, tarehe za kuanza na za kuisha, jina la mwenye bima, na maelezo ya gari ikiwa ni pamoja na nambari ya utambulisho wa gari.

9. Leseni yako itatolewa baada ya wewe kupita mtihani wa barabarani, kulipa ada zinazohitajika na kutoa kitambulisho sahihi (tazama Sura ya 3).

**Kuhamisha Leseni ya Dereva kijana nje ya Jimbo (waombaji wa umri wa chini ya miaka 18)**

Unaweza kubadilisha Leseni ya Dereva Kijana nje ya jimbo na kupata Leseni ya Dereva Kijana ya Vermont kwa: (1) kufaulu mitihani inayohitajika; (2) kutoa uthibitisho (tazama Nahitaji Nini ili kupata Leseni ya Dereva Kijana?, #2 hapo juu) wa kukamilisha kwa mafanikio mpango wa Elimu ya Dereva ulioidhinishwa na serikali; (3) kutoa uthibitisho wa kamilisho la saa 40 za ziada za kuendesha gari.

Kama una Leseni ya Dereva Kijana kutoka jimbo lingine na uombe Leseni ya Dereva Kijana ya Vermont utakuwa chini ya masharti ya Leseni ya Hatua kwa Hatua ya Vermont isipokuwa iwe umekuwa na Leseni ya Dereva Kijana katika jimbo lingine kwa kipindi cha angalau miezi sita.

**Mtihani wa Leseni ya Udereva wa Shule ya Upili**

Baadhi ya wakufunzi wa elimu ya udereva wa shule za sekondari wenye leseni ya DMV husimamia majaribio ya barabarani ya Leseni ya Udereva. Huduma hii hutolewa tu katika shule ambazo zimejiandikisha katika mpango wa jaribio, na wale wakufunzi ambao wamethibitishwa kama wakaguzi na

Idara ya Magari. Majaribio ya barabarani yatatolewa tu kwa wanafunzi wanaohudhuria shule inayoshiriki.

Mwanafunzi aliyefaulu jaribio la barabarani lililotolewa na mwalimu wa elimu ya udereva wa shule ya upili atapewa **Cheti cha Mtihani wa Elimu ya Udereva.** Cheti hiki, Kibali halali cha Mwanafunzi wa Vermont, maombi ya leseni yaliyokamilishwa na kutiwa saini na mzazi au mlezi wa kisheria, ada ya jaribio la barabarani na ya leseni, na thibitisho la makazi ya Vermont vyote vinahitajika kwa utoaji wa leseni. Hizi lazima ziwasilishwe moja kwa moja kwa Ofisi yoyote ya Huduma ya Wateja wa Gari. Walimu katika shule zinazoshiriki watatoa habari kamili kuhusu mpango huu kwa wanafunzi.

**Ni vikwazo gani vilivyo kwenye Leseni ya Dereva Kijana?**

Leseni ya Dereva Kijana inachukuliwa kuwa leseni ya muda. Kamishna wa Magari anaweza kuchukua leseni yako ukionyesha kuwa wewe ni dereva asiye salama kupitia vitendo vyako. Leseni yako inaweza pia kuchukuliwa ikiwa mzazi au mlezi wako atakuondolea ruhusa ya wewe kuendesha gari.

Ukiwa na Leseni ya Dereva Kijana, **huwezi** kuendesha gari wakati wa ajira yako kwa mwaka mmoja (1) kufuatia kupewa Leseni ya Dereva Kijana. Kwa mfano, mtu hawezi kufanya kazi ya mpeleka pizza (dereva) hadi awe na Leseni ya Dereva Kijana kwa mwaka mmoja (1), au hadi afikie umri wa miaka kumi na nane (18), lolote linalofika kwanza.

Wakati anamiliki Leseni ya Dereva Kijana, mtu hawezi kubeba abiria wa kukodisha.

Katika miezi tatu (3) ya kwanza ya udereva akiwa na Leseni ya Dereva Kijana, mtu huyo anazuiwa kuendesha gari peke yake. Abiria wanaruhusiwa tu kama kuna mzazi au mlezi mwenye leseni na asiyedhurika, au mwalimu wa elimu ya udereva mwenye leseni au aliyeidhinishwa na asiyedhurika au mtu mwenye leseni na asiyedhurika mwenye umri wa miaka 25 au zaidi anayebebewa kiti cha mbele. Ikiwa mmoja (1) wa watu hao yuko kwenye gari, hakuna kizuizi kwa idadi ya abiria. Hata hivo, dereva **haruhusiwi** kusafirisha abiria wengi zaidi kuliko mikanda ya usalama.

Katika kipindi cha miezi tatu (3) ya pili ya uendeshaji gari na Leseni ya Dereva Kijana, mtu huyo anaweza kuanza kusafirisha wanafamilia .

Baada ya kumiliki Leseni ya Dereva Kijana kwa miezi sita (6), hakuna kizuizi kuhusu idadi ya abiria anaoweza kusafirisha kwenye gari. Hata hivyo, dereva haruhusiwi kusafirisha abiria wengi zaidi kuliko mikanda ya usalama.

Mtu hatatumia kifaa chochote cha elektroniki kinachobebeka wakati wa kuendesha gari. Hii ni pamoja na kusoma, kuandika kwa mkono au kutuma mawasiliano ya elektroniki (ikiwa ni pamoja na ujumbe wa maandishi, ujumbe wa papo hapo, na barua pepe). Vifaa vya elektroniki vinavyobebeka ni pamoja na, lakini sio tu, simu za mkononi, kisaidizi cha kidijitali cha kibinafsi (PDA), kompyuta kibao/iPad na kompyuta mpakato.

## Maswali na Majibu Kuhusu Leseni za Dereva Ni Nani

### Anaweza Kupata Leseni ya Dereva?

Leseni ya Udereva hutolewa kwa watu wenye umri wa miaka 18 au zaidi ambao wamepita mtihani unaohitajika. Leseni hii humruhusu mtu kuendesha gari lolote lisilo la kibiashara isipokuwa basi la shule au pikipiki. Ili kuendesha basi la shule au kuendesha pikipiki mitihani ya ziada inahitajika.

### Ninawezaje kupata Leseni ya Udereva kama nina Kibali Halali cha Mwanafunzi?

1. Weka miadi kwa ajili ya mtihani.
2. Kuwa na mzazi au mlezi mwenye leseni na asiyedhurika, au mwalimu wa elimu ya udereva aliye na leseni au aliyethibitishwa na asiyedhurika, au mtu mwenye leseni na asiyedhurika mwenye umri wa miaka 25 au zaidi awe pamoja nawe. Leseni ya dereva yeyote unayeandamana naye lazima iwe halali wakati wa maombi.
3. Kuwa na gari ambalo ni safi na katika hali nzuri ya mitambo na liwe na kibandiko halali cha ukaguzi. Hakikisha kuwa breki ya dharura/ya kuegesha inafanya kazi vizuri.
4. Thibitisho la bima halali na ya sasa ya gari inahitajika na sheria ya Vermont. Thibitisho lazima lieleze jina la mtoa huduma ya bima, tarehe za kuanza na za kumalizika kwa bima, jina la mwenye bima, maelezo ya gari ikiwa ni pamoja na nambari ya utambulisho wa gari.
5. Thibitisho la usajili halali wa gari linahitajika.
6. Leseni yako itatolewa baada ya kupita jaribio la barabarani na kulipa ada.

### Ninawezaje kupata Leseni ya Dereva kama nina leseni halali kutoka jimbo lingine?

Wakati Mkazi mpya wa **Vermont** anaomba Leseni ya Udereva ya Vermont na ana leseni halali ya nje ya jimbo au leseni ya nje ya jimbo ambayo muda wake wa kuisha ni miaka mitatu (3) au chini, uchunguzi wa macho utahitajika.

1. Leta leseni yako halali au iliyoisha (miaka 3 au chini) kutoka kwa Jimbo lako, thibitisho la utambulisho (tazama sura ya 3). Kama leseni ya Jimbo lako si halali, uwe na mtu ambaye ana leseni halali atakayekuendesha kwa Idara ya Magari. Kama leseni yako imeisha kwa zaidi ya miaka mitatu (3), au huna leseni ya nje ya jimbo, itabidi ufanya mtihani wa kuangalia, wa maandishi na wa barabarani.

### Ni Nani Hawezi Kupewa Leseni Mpya au kufanya Upya Leseni Yake?

Mtu ambaye haki yake ya kuendesha gari katika jimbo lolote imesimamishwa, kufutwa, au kukataliwa hawezi kupewa leseni hadi kusimamishwa, kuondolewa au kukataliwa huko kumesitishwa na mtu huyo amearifiwa rasmi kwa maandishi kuhusu kurejeshwa.

Leseni haiwezi kutolewa kwa mtu wakati Kamishna wa Magari ana ushahidi kwamba mtu huyo hawezi au hataendesha gari bila kuhatarisha watumiaji wengine wa barabara kuu.

Mtu ambaye si Mkazi wa Vermont.

## KUIDHINISHWA KWA BASI LA SHULE

Kila dereva mwenye leseni ya Vermont, ambaye husafirisha watoto wa shule katika basi la shule, lazima awe na leseni ya udereva na idhinisho la basi la shule.

- Ikiwa unaendesha basi la shule, ambalo lina jumla ya uzito wa gari wa ratili 26,001 au zaidi, au ambalo limetengenezwa kubeba abiria 16 au zaidi pamoja na dereva, utahitaji Leseni ya Dereva ya Biashara yenye idhinisho ya abiria na shule.
- Kama unasafirisha watoto wa shule kwa mabasi ya shule yaliyotengenezwa kubeba abiria chini ya 16, unahitajika kupata idhinisho la basi la shule la Aina ya II kwenye leseni yako ya dereva.
- Kama unasafirisha watoto wa shule kwa magari mengine, unaweza pia kuhitaji idhini ya basi la shule ya Aina ya II.
- Kama unasafirisha watoto wa shule kwa basi la shughuli nyingi za shule, linalomilikiwa au kukodishwa na shule, unahitaji idhini ya basi la shule.
- Kama unasafirisha watoto wa shule kwa kukodiwa, kama vile kwenye teksi, lazima uwe na idhini ya basi la shule.
- Kama unasafirisha watoto wa shule kwa magari madogo au vani yanayomilikiwa kibinafsi au na shule, unaweza kuhitajika kupata idhini ya basi la shule kwenye leseni yako ya dereva.

Unaweza kupata mwongozo wa basi la shule kwa kutembelea mojawapo ya ofisi zetu.

## IDHINI ZA PIKIPIKI NA VIBALI VYA MWANAFUNZI VYA PIKIPIKI

Mtu yeyote mwenye umri wa miaka 16 au zaidi ambaye ana leseni anaweza kupata idhinisho la pikipiki au kibali cha pikipiki kwa kupita mtihani.

Unapaswa kusoma **Mwongozo wa Leseni ya Pikipiki na Mwongozo wa Mwendeshaji** kabla ya kufanya mtihani. Unaweza kupata mwongozo wa pikipiki kwa kutembelea mojawapo ya ofisi zetu.

## PROGRAMU YA MAFUNZO YA MWENDESHA PIKIPIKI

Programu ya Elimu ya Mwendesha Pikipiki ya Vermont (VREP) inahimiza watu wa umri wote ambao wanapenda kuendesha pikipiki kufanya mafunzo haya. Programu ya mafunzo hufuata viwango vya usalama na mafunzo vinavyotambuliwa kitaifa na inahusisha mafunzo ya darasani na ya pikipiki. Pikipiki, vitabu vya kiada, na helmeti hutolewa kwa wanafunzi wanaofanya Kozi ya Msingi ya Mwendesha Pikipiki. Wanafunzi ambao wamefanikiwa kukamilisha kozi hiyo hawapaswi kufanya mitihani ya jimbo ya maandishi na ya ustadi inayohitajika kupata idhinisho la pikipiki. Kwa habari ya kozi tembelea tovuti ya DMV ya Vermont.

## Je, ninahitaji Miadi?

Ndiyo, tembelea mydmv.vermont.gov ili kupanga miadi. Ziara zote za DMV ni kwa miadi tu. Kama huwezi kuweka miadi iliyopangwa, tafadhali ghairi au upange upya miadi yako haraka iwezekanavyo ili tuweze kuratibu kwa mtu mwingine muda uliopangwa. Angalia uthibitisho wako wa bima halali kama inavyohitajika na Sheria ya Vermont na usajili wa gari kabla ya kuwasili DMV.

**Kumbuka:** Kama una tatizo la kusikia mkalimani ataandaliwa ikiwa ataombwa wakati wa kupanga miadi. Huduma ya Ulemavu wa kuwasiliana ya Vermont (TTY) inapatikana kwa kupiga simu 711.

## Kwa Nini Serikali Inahitaji Mtihani wa Kuendesha Gari?

Mitihani hutumiwa kutathmini yafuatayo:

- Unaweza kusoma na kuelewa alama za barabarani na taa zinazotumiwa barabarani?
- unajua sheria kuhusu kuendesha magari katika jimbo hili?
- Unaweza kuona vizuri ili kuendesha gari kwa salama?
- Una ujuzi sahihi wa kuendesha gari ili kukuwezesha kuwa dereva salama na mwenye hashima?
- Una ulemavu wowote unaoweza kuathiri uwezo wako wa kuendesha gari lako kwa usalama?
- Utatunza vizuri gari lako ili liwe salama kuendesha?
- Uko tayari na una maarifa yanayohitajika kuwa dereva salama na mwenye heshima?
- Umekubali kuheshimu haki za waendesha baiskeli, waendesha pikipiki, na watembea kwa miguu pamoja na madereva wengine?

## Mitihani hiyo ikoje?

1. **Mtihani wa Macho**

   Kwa kutumia kifaa cha kuchunguza macho, mtahini atapima uwezo wako wa kuona vizuri. Ikiwa matokeo ya uchunguzi yataamua kuwa kuona kwako hakufikii viwango vinavyohitajika vya 20/40, utatumwa kwa daktari wa macho unayependelea na gharama yako kwa upimaji zaidi. Daktari wa macho atakamilisha tathmini ili kuamua kama vizuizi vyovyote vinapaswa kuwekwa kwenye haki yako ya kuendesha gari. Daktari wa macho lazima awe na leseni ya kupima macho au mtaalamu wa kuchunguza macho.

2. **Mtihani wa maarifa**

   Mtihani wa maarifa uko mtandaoni na una maswali 20. Kila swali lina majibu manne ya kuchagua , ambayo moja tu ndiyo sahihi. Lazima ujibu angalau maswali 16 kwa usahihi ili kupita mtihani. Ukifeli mtihani, lazima usubiri angalau siku moja kabla ya kufanya mwingine.

3. **Jaribio la Barabarani**

   Jaribio la barabarani halitatolewa hadi utakapopita sehemu zingine zote za mtihani.

   Kabla ya mtihani, unapaswa kuwa na angalau saa 40 ya uzoefu halisi wa kuendesha gari chini ya uongozi wa dereva mwenye uzoefu au mwalimu wa udereva. Angalau saa tano za hizi zinapaswa kuwa katika trafiki. Kwa kawaida kila mtu mwenye uwezo wa wastani na mazoezi ya kutosha, chini ya usimamizi wa mwalimu mzuri, anaweza kujifunza kuendesha gari.

Katika jaribio la barabarani, hutaambiwa ufanye chochote ambacho ni kinyume cha sheria. Hakuna hila zitachezwa kwako. Lazima ufuate maelekezo ya mtahini ambaye atakuwa garini pamoja nawe. Utatarajiwa kushughulikia gari lako kwa ustadi, kuendesha gari kwa kasi inayofaa kulingana na hali, na kutii ishara na sheria za barabara.

Wanyama hawaruhusiwi kwenye gari wakati wa jaribio la barabarani.

Ukifeli jaribio la barabarani kwa sababu yoyote ile, lazima usubiri angalau wiki moja kabla ya kufanya mtihani mwingine. Ukifeli jaribio la barabarani mara tatu, muda wa chini wa kusubiri wa mwezi mmoja unahitajika.

## Ninapaswa Kuwa na Gari ninapofanya mtihani wa Kuendesha Gari?

**Ndiyo.** Gari linapaswa kusajiliwa na kukaguliwa. Jimbo ambalo limesajiliwa na kukaguliwa haijalishi. Lazima uwe na thibitisho la bima la gari unalotumia. Angalia usajili wako, kibandiko cha ukaguzi na bima kabla ya kufika kwa mtihani.

Magari ya kukodisha hayawezi kutumika kwa majaribio ya barabarani isipokuwa kampuni ya kukodisha itoe barua inayokubali daraka kamili ikiwa mwombaji atafanya jaribio la barabarani katika gari la kukodisha. Magari ambayo yanaonyesha usajili wa muuzaji hayakubaliki isipokuwa wewe ni mwanafamilia wa karibu wa muuzaji. Hakuna jaribio la barabarani litakatolewa katika gari lenye bamba za kilimo, za tunu au za maonyesho kwa sababu bamba hizi, kwa sheria, zimezuiliwa katika matumizi yazo.

## Hali ya Gari Linalotumika katika Jaribio la Barabarani

Hutaruhusiwa kufanya mtihani wa kuendesha gari ila tu gari unalotumia lina vifaa vizuri, katika hali nzuri ya mitambo, na kusajiliwa ipasavyo, lina bima, na limekaguliwa. Hali salama ya uendeshaji wa gari ni wajibu wa mwendeshaji. Vifaa sahihi katika hali nzuri ya mitambo ni pamoja na: taa za mbele, honi, waipa ya kioo cha mbele, kioo cha kutazama nyuma, taa za nyuma, matairi, usukani, kioo cha mbele, mfumo wa ekzosi, breki, madigadi, bamba na kama ilitengenezwa au kuunganishwa baada ya Januari 1, 1955, ishara za mwelekeo. Mikanda ya usalama na viondoaukungu vinahitajika katika magari ya 1964 na baadaye. Hakuna jaribio la barabarani litatolewa katika gari ambalo halina mikanda ya usalama. Breki za dharura /za kuegesha lazima ziweze kushikilia gari kwenye gia huru kwa daraja lolote ambalo linaendeshwa, iwe gari linaelekea mlimani au mteremko. Kutia rangi ya kivulivuli kinyume cha sheria kwa madirisha ya mbele ya gari lako hakuruhusiwi

# Sura ya 5 - Mpango wa Leseni ya Udereva ya Hatua kwa Hatua

## Mpango wa Leseni ya Udereva ya Hatua kwa Hatua

Watu ambao wanapata Kibali cha Mwanafunzi au Leseni ya Dereva Kijana wako chini ya sheria yetu ya Leseni ya Udereva ya Hatua kwa Hatua. Masharti muhimu ya sheria hii yanaonyeshwa hapa chini:

1. Mtu mwenye umri wa miaka kumi na mitano (15) au zaidi anaweza kuendesha gari akiwa ana Kibali halali cha Mwanafunzi na akiandamana na mojawapo (1) ya watu wafuatao kwenye gari, ambaye ataketi kando ya dereva:
    - Mzazi au mlezi mwenye leseni na asiyedhurika,
    - Mwalimu wa elimu ya udereva aliye na leseni au aliyethibitishwa na asiyeadhurika, na/au
    - Mtu mwenye leseni na asiyedhurika aliye na angalau **miaka ishirini na mitano (25).**
2. Ili kutuma ombi la Kibali cha Mwanafunzi, mtu lazima awe na rekodi safi ya kuendesha gari katika miaka miwili (2) iliyopita
3. Mtu lazima awe na Kibali cha Mwanafunzi kwa angalau mwaka mmoja (1) kabla ya kupata Leseni ya Dereva Kijana.
4. Kabla ya kupata Leseni ya Dereva Kijana, mtu lazima akamilishe saa arobaini (40) za ziada za mazoezi ya kuendesha gari, na angalau masaa saa kumi (10) za kuendesha gari usiku, huku akiandamanana na mojawapo ya watu waliotajwa hapo juu ambao wanaketi kando ya dereva. Saa arobaini (40) za mazoezi ni pamoja na saa sita za kuendesha gari unaohitajika ili kukamilisha kwa mafanikio kozi ya mafunzo ya udereva. Mazoezi haya ya ziada lazima yathibitishwe na mmoja wa watu waliotajwa hapo juu. KUMBUKA: 'Kuendesha gari usiku' hufafanuliwa kama kuendesha gari wakati wa dakika thelathini (30) baada ya jua kutua, hadi dakika thelathini (30) kabla ya mapambazuko.
5. Mtu lazima awe amedumisha rekodi 'safi' ya kuendesha gari bila Kibali chake cha Mwanafunzi kusitishwa wakati wowote, kusimamishwa, au kubatilishwa kwa kipindi cha miezi sita (6) kabla ya kupata Leseni ya Dereva Kijana.
6. Huku akiwa na Leseni ya Dereva Kijana, mtu huyo hawezi kuendesha gari wakati wa ajira yake kwa mwaka mmoja (1) kufuatia utoaji wa Leseni ya Dereva Kijana. Kwa mfano, mtu hawezi kufanya kazi ya dereva mpeleka pizza hadi awe na Leseni ya Dereva Kijana kwa mwaka mmoja (1), au hadi atimize umri wa miaka kumi na nane (18), lolote linalotangulia.
7. Wakati anamiliki Leseni ya Dereva Kijana, mtu hawezi kubeba abiria wa kukodisha.
8. Katika miezi tatu (3) ya kwanza ya udereva akiwa na Leseni ya Dereva Kijana, mtu huyo anazuiwa kuendesha gari peke yake. Abiria wanaruhusiwa tu kama kuna mzazi au mlezi mwenye leseni na asiyedhurika, au mwalimu wa elimu ya udereva mwenye leseni au aliyeidhinishwa na asiyedhurika au mtu mwenye leseni na asiyedhurika mwenye umri wa miaka 25 au zaidi anayebebewa kiti cha mbele. Ikiwa mmoja (1) wa watu hao yuko kwenye gari, hakuna

vikwazo kwa idadi ya abiria. Hata hivyo, dereva haruhusiwi kusafiri na abiria wengi kuliko mikanda iliyopo ya usalama.

9. Wakati wa miezi mitatu (3) ya pili ya udereva akiwa na Leseni ya Dereva Kijana, mtu huyo anaweza kuanza kusafirisha wanafamilia wa karibu; wazazi na ndugu zake pekee.

10. Baada ya kumiliki Leseni ya Dereva Kijana kwa miezi sita (6), hakuna kizuizi kuhusu idadi ya abiria anaoweza kusafirisha kwenye gari. Hata hivyo, dereva haruhusiwi kusafiri na abiria wengi kuliko mikanda iliyopo ya usalama.

11. Mtu anayemiliki Leseni ya Dereva Kijana ya Vermont lazima awe na umri wa miaka kumi na minane (18) na isikuwe ina kusitishwa kwokwote, kusimamishwa, au kubatilishwa kwa kipindi cha miezi sita (6) iliyopita, ili kustahili kupata Leseni ya Dereva. Kipindi hiki cha miezi sita (6) huanza tarehe ya kurejeshwa.

12. Mtu anayemiliki Leseni ya Dereva Kijana kutoka jimbo lingine anapoomba Leseni ya Dereva Kijana ya Vermont, atahitajika kutoa thibitisho kwamba amekamilisha kwa mafanikio kozi ya elimu ya udereva iliyoidhinishwa na serikali ambayo inakidhi au kuzidi masharti ya Vermont. Pia atahitajika kupita mtihani wa upimaji macho, wa maandishi na wa barabarani. Pia atakuwa chini ya Sheria ya Leseni ya Hatua kwa Hatua ila tu awe mmiliki wa leseni ya lile jimbo lingine kwa kipindi cha angalau miezi sita.

13. Kibali cha Mwanafunzi au Leseni ya Dereva Kijana huchukuliwa kuwa ' leseni ya muda', ambayo hubatilikika. Yoyote ya vitendo vifuatavyo vitasababisha kusitishwa kwa Kibali cha Mwanafunzi cha mtu binafsi au Leseni ya Dereva Kijana (**kwa maelezo zaidi, angalia 23 VSA § 607a, § 614a**):

    - Kubeba Abiria wa Kukodisha, Ukiukaji wa Dereva Kijana (CPH) = kusitishwa siku 90
    - Kumwendeshea Mwajiri Gari/Ajira, Ukiukaji wa Dereva Kijana (DFE) = Kusitishwa siku 90
    - Mapendekezo Kutoka kwa Bodi ya Mchepuo/Urekebishaji na Bodi ya Kurekebisha (DRB) = Kusitishwa siku 30
    - Uzuiliwaji wa Mkusanyo wa Pointi za Dereva Kijana (JRP) = Kusitishwa siku 90 (pointi 3 Kwa Ukiukaji wa Mwendo Kasi mmoja au pointi 6 kwa Jumla)
    - Dereva Kijana kutuma ujumbe mfupi (JRT) = Kusitishwa siku 30 (inajumuisha faini ya angalau $100 na angalau pointi mbili kwenye rekodi yako ya udereva)
    - Wakati kusitishwa kunaendelea, mtu **hastahili** kupata Leseni ya Dereva Kijana au Leseni ya Dereva.
    - Wakati kusitishwa kunatolewa, mtu ana haki ya kusikilizwa.
    - Wakati Kibali cha Mwanafunzi au Leseni ya Dereva Kijana imesitishwa, itarejeshwa baada ya kumalizika kwa muda maalum, na, ikiwa itahitajika, wakati mtu huyo amepita mtihani wa marudio.
    - Hakuna ada ya kurejesha italipwa wakati Kibali cha Mwanafunzi/ Leseni ya Dereva Kijana iliyositishwa itarejeshwa.

*Ajali za magari ndizo sababu kuu ya vifo na majeraha kwa vijana. Kama mzazi au mlezi, una jukumu muhimu la kushawishi tabia salama za mtoto wako za kuendesha gari.*

Waendesha baiskeli ni watumiaji halali wa barabara na wana haki na wajibu sawa na madereva wa magari mengine. Ingawa leseni haihitajiki kuendesha baiskeli, waendesha baiskeli wanapaswa kufuata sheria zote za barabarani. Waendesha baiskeli wanaruhusiwa kuendesha wawili sambamba ili mradi tu hawazuii mwendo wa kawaida na unaofaa kwa magari. Fuata sheria zifuatazo kwa uzoefu salama na wa kisheria wa kuendesha baiskeli:

- Tii ishara na alama zote za barabara. Ukivunja sheria zozote za trafiki, utapewa tikiti na faini.
- Endesha pamoja na magari. Daima endesha pamoja na magari kwenye upande wa kulia wa barabara. Ukikaribia njia ya kugeukia kulia na unakusudia kuendelea moja kwa moja, usiingie kwenye njia ya kugeukia kulia
- Endesha gari kwa njia ya kutabirika. Daima endesha kwa mstari ulionyooka; usipinde na kutoka ndani na nje ya magari yaliyoegeshwa. Kama barabara ni nyembamba sana kwa baiskeli na gari kusafiri sambamba, mwendesha baiskeli anapaswa kufuata njia hadi iwe salama kurudi kulia. Angalia huku na huku kabla ya kubadilisha nafasi yako ya njia na usipenye kati ya magari yaliyoegeshwa.
- Weka ishara za kugeuka. Lazima kila wakati uonyeshe nia yako ya kugeuka, kwa kutumia ishara sahihi za mkono. Angalia ili kuhakikisha njia ziko wazi kwa magari kabla ya kubadilisha njia au kugeuka.

- **Ishara za Mkono kwa Waendesha Baiskeli**



**Kushiriki Barabara na Watelezi kwa ubao, Skuta, n.k.**

Wasiwasi maalum wa hivi karibuni ni watumiaji wa usafiri binafsi wenye magurudumu kama vile wateleza kwa ubao, wapanda rola sketi, skuta zisizo na injini, viti vya magurudumu vya umeme, n.k. Watu wanaotumia barabara na vifaa hivi wakati mwingine wanaweza kuwa wakisafiri kwa kasi kubwa. Watumiaji wanaweza kusogea ghafla na kubadilisha mwelekeo bila kutarajiwa kwenye njia yako ya safari. Kuwa makini zaidi na tahadhari hasa karibu na watumiaji wa barabara wa aina hii.

**Kushiriki Barabara na Pikipiki**

Waendesha pikipiki wa leo ni marafiki, jamaa na majirani. Mwendesha pikipiki ana haki na wajibu sawa barabarani kama madereva wa magari mengine. Madereva wanapaswa kutambua hili na sio kujaribu kuzizuia pikipiki au kuwanyima waendesha pikipiki haki ya kupita. Waendesha pikipiki kwa upande mwingine lazima waendeshe kama watumiaji wa barabara wenye uwajibikaji na wasijaribu kutumia upenyo wa umbo dogo la pikipiki na uwezo wake wa kugeuka kwa urahisi.

Waendesha pikipiki mara nyingi hupunguza mwendo kwa kubadili gia au kupunguza mwendo wa injini, hivyo hawawashi taa za breki. Ruhusu zaidi ya sekunde 4 za umbali wa kufuata. Kwenye makutano, chukulia kuwa mwendesha pikipiki anaweza kupunguza mwendo bila onyo la kuona.

Ishara za kugeuka kwenye pikipiki kawaida hazizimiki zenyewe, hivyo waendesha pikipiki, (hasa wanaoanza) wakati mwingine husahau kuzima baada ya kugeuka au kubadilisha njia. Hakikisha kuwa ishara ya pikipiki ni ya kweli.

Waendesha pikipiki mara nyingi hubadilisha nafasi ndani ya njia ili kuonekana kwa urahisi zaidi na kupunguza athari za upepo, uchafu wa barabara, na magari yanayopita. Elewa kuwa waendesha pikipiki hubadilisha barabara kwa sababu maalum, sio kwa sababu ya kutojali au kujionyesha.

Kwa sababu ya udogo wake pikipiki huonekana inaenda haraka kuliko ilivyo.
Usifikiri kuwa waendesha pikipiki ni pepo wa kasi.

Kwa sababu ya udogo wake, pikipiki inaweza kuonekana kuwa mbali zaidi kuliko ilivyo. Unapopeleleza trafiki ili kugeuka kwenye makutano, chukulia kuwa pikipiki iko karibu kuliko inavyoonekana.

Kwa sababu ya udogo wake, pikipiki inaweza kufichwa kwa urahisi na vitu vilivyo ndani au nje ya gari (nguzo za milango, vioo, abiria, vichaka, miti, magari yaliyoegeshwa, ua, madaraja, maeneo yaliyofichika, nk). Chukua muda wa ziada kukagua trafiki kwa kina, iwe unabadilisha njia au unageuka kwenye makutano.

Umbali wa kusimama wa pikipiki ni karibu sawa na wa magari, lakini barabara telezi hufanya kusimama kuwa ngumu. Ruhusu umbali zaidi wa kufuata nyuma ya pikipiki kwa sababu haiwezi kusimama "kimiujiza".

Uwezo wa kugeuka kwa urahisi ni moja ya sifa bora za pikipiki, hasa wakati wa mwendo wa polepole na hali nzuri za barabara. Lakini usitarajie mwendesha pikipiki kuwa na uwezo wa kukwepa kila wakati.

Kubeba abiria kunatatiza kazi ya mwendesha pikipiki. Kuweka usawa ni vigumu zaidi. Umbali wa kusimama huongezeka. Uwezo wa kugeuka kwa urahisi hupungua. Chukulia kuwa kuna matatizo zaidi unapoona watu wawili kwenye pikipiki, hasa karibu na makutano.

Vioo ni vidogo kwenye pikipiki na kawaida ni vya kubinuka. Hii humpa mwendesha pikipiki picha ndogo yako na kukufanya kuonekana uko mbali zaidi kuliko ulivyo. Ruhusu angalau nafasi ya sekunde nne unapofuata mwendesha pikipiki.

Kuna magari na malori mengi kuliko pikipiki barabarani, na baadhi ya madereva "hawatambui" pikipiki na ila huipuuza (kwa kawaida bila kukusudia). Pekua pikipiki, hasa unapopeleleza magari kwenye makutano.

Usiku, taa za mbele na taa za nyuma kwenye pikipiki zinaweza kuchanganyika na taa za magari mengine. Taa hizo "zisizo za kawaida" zinaweza kuwa za pikipiki.

Pikipiki zina haki ya kuwa kwa njia nzima. Wakati wa kupita pikipiki, badilisha njia kabisa. Kamwe usijipachike karibu sana mara tu unapita pikipiki. Hakikisha unatumia ishara zako za kugeuka ili kumtahadharisha mwendesha pikipiki kuhusu nia yako ya kupita, kubadilisha njia au kugeuka. Mpe mwendesha pikipiki anayepita nafasi ya kutosha na usijaribu kuongeza kasi ili kukaa mbele ya pikipiki inayokupita.

Wakati pikipiki inasonga, usiifikirie kuwa pikipiki; ifikirie kuwa mtu.

**Kumbuka:** Maelezo zaidi kuhusu sheria na kanuni za pikipiki, na jinsi ya kupata leseni ya pikipiki au idhini, yanaweza kupatikana katika Mwongozo wa Pikipiki wa Vermont.

## Kushiriki Barabara na Malori Makubwa

Kila mwaka kuna zaidi ya ajali 250,000 zinazohusisha magari ya abiria na malori makubwa. Katika zaidi ya 70% ya ajali mbaya zinazohusisha magari na malori, dereva wa lile gari lingine, sio dereva wa lori, alisababisha ajali. Ajali nyingi zinazohusisha magari na malori hutokea mchana kwenye barabara nyoofu na kavu katika hali nzuri ya hewa. Malori ni makubwa na mazito kuliko magari mengine. Katika ajali nne kati ya tano zilizohusisha malori, dereva wa hilo gari jingine aliuawa. Nyingi za ajali hizi zingeepukwa kama waendesha magari wangejua kuhusu mapungufu ya lori na jinsi ya kuondokea hali zisizo salama kuhusu malori.




**Kumbuka, malori hayaendeshwi kama magari mengine. Kwa ujumla, kadiri lori lilivyo kubwa:**

- Ndivyo maeneo fiche ya dereva yanavyokuwa makubwa zaidi.
- Ndivyo lori linavyohitaji nafasi zaidi ili kubadilisha mwelekeo.
- Ndivyo inavyochukua muda mrefu zaidi kwa lori kusimama.
- Ndivyo inavyochukua muda mrefu zaidi kwako kuipita.

## TAHADHARI MAENEO FICHE—"MAENEO YASIOONEKANA"

Malori makubwa yana maeneo fiche, au Maeneo Yasioonekana, karibu na mbele, nyuma na pande za lori. Lori inaweza hata kukugeukia, kwa sababu haya Maeneo Yasioonekana hufanya iwe ngumu kwa dereva kuona. Usikae katika Maeneo Yasioonekana. Kumbuka, kama huwezi kuona vioo vya (upande) kutazama nyuma vya lori basi dereva wa lori hawezi kukuona.

## Kupita

Huchukua muda mrefu kupita gari kubwa. Unapaswa kudumisha kasi thabiti wakati wa kupita. Hakikisha unaweza kuona sehemu ya mbele ya lori kwenye kioo chako cha ndani cha kutazama nyuma kabla ya kurudi kwenye njia ya kulia. Magari yanapoingia mbele ya lori haraka sana, huenda dereva wa lori akalazimika kuchukua hatua haraka ili kuepuka ajali.

## Kurudi Nyuma

Wakati dereva wa lori anaporudi nyuma, wakati mwingine analazimika kuziba barabara kwa muda ili kugeuza trela lake. Kamwe usijaribu kupita lori linalojiandaa kurudi nyuma au lililoko katika mchakato wa kurudi nyuma. Trela nyingi zinaweza kuficha kabisa vitu vinavyojitokeza ghafla

kati yake na eneo la upakiaji. Ukijaribu kuzunguka lori, unaweza kuingia eneo fiche na dereva wa lori hawezi kukuona.

**Maeneo Fiche ya Nyuma**

Tofauti na magari mengine, malori yana maeneo marefu fiche moja kwa moja nyuma yao. Dereva wa lori hawezi kuona gari lako katika nafasi hii, na mtazamo wako wa mkondo wa magari hupunguka sana. Kufuata kwa karibu sana huongeza nafasi yako ya mgongano wa nyuma na lori. Kama huwezi kuona vioo vya kutazama nyuma vya lori basi dereva wa lori hawezi kukuona.

**Maeneo Fiche ya Upande**

Malori yana maeneo kubwa zaidi fiche kwenye pande zote mbili za magari yao kuliko magari ya abiria. Unapoendeshea gari maeneo haya fiche kwa muda wowote, huwezi kuonekana na dereva wa lori. Kama dereva wa lori anahitaji kubadilisha njia haraka kwa sababu yoyote, ajali mbaya inaweza kutokea kama gari lako liko katika eneo fiche la dereva wa lori.




**Kugeuka Upana**

Daima angalia ishara za kugeuka za lori. Madereva wa malori mara nyingi wanahitaji mzunguko wa upana upande wa kushoto ili kufanya geuko la kulia. Hawawezi kuona magari nyuma au kando yao. Usipenye kati ya lori na ukingo au pembezoni mwa barabara upande wa kulia; hii huongeza uwezekano wa ajali.

**Kushiriki Barabara na Magari ya Kwenda Polepole**

Gari linaloenda polepole, kama vile trekta au mashine nyingine kubwa ya kilimo haliwezi kusafiri kwa kasi kwenye barabara kuu. Linatambuliwa na ishara ya rangi za chungwa na nyekundu ya pembe tatu iliyowekwa nyuma ya gari. Ishara hizi husaidia waendesha magari kutambua gari lililo mbele kwa haraka zaidi. Kadiri unavyoweza kutambua gari linalosonga polepole ndivyo ulivyo na wakati mwingi wa kuweza kupunguza kasi yako. Magari ya kwenda polepole yanaweza kufanya mageuko mapana kwenye viingilio visivyo na alama upande wa kulia au kushoto wa barabara. Baadhi ya vifaa vya kilimo ni vipana kuliko barabara yenyewe.



Baadhi ya magari, au vifaa, yanaweza kuyumba kwenye barabara na huenda usiweze kuona dereva.

Unapoendesha gari linalosonga polepole ambalo linasababisha ucheleweshaji wa magari, unaweza kuliegesha kando ya barabara, ikiwa na iwapo inawezekana na ni salama kufanya hivyo, ili kuruhusu wengine kusafiri kwa usalama. Waendeshaji wa magari ya kilimo wana haki ya kuendeshea magari yao barabarani. Dumisha umbali salama wa kufuata magari ya mwendo wa polepole ili mwendeshaji aweze kukuona, au uweze kumuona, kama inawezekana. Inaweza kuwa muhimu kuruhusu zaidi ya sekunde nne za umbali wa kufuata. Vipishe vifaa vipana kwenye barabara nyembamba. Pita magari yanayoenda polepole kwa tahadhari, na kama tu hali ni salama, na hakuna magari yanayokuja. Kuwa mvumilivu na uwe mwangalifu kwa magari yanayoweza kugeuka. Shiriki barabara kwa usalama na magari makubwa na ya mwendo wa polepole. Tazama "Kuweka Barabara zetu za Vijijini Salama huko Vermont."



**Madereva Jeuri**

Madereva jeuri huenda hawafikirii matokeo ya matendo yao wanapoendesha magari kwa kasi sana na kupita wakati usio salama. Wanaweza kukosa kutumia ishara za kubadilisha njia na wanaweza kuingia na kutoka kwa trafiki, hufuata kwa karibu sana na kuyazuia magari yanapojaribu kwenda mbele. Vitendo vyote hivi ni vya kinyume cha sheria na vinaweza kusababisha tiketi za trafiki au madhara zaidi. Madereva jeuri wanaweza pia kupiga kelele, kupiga honi zao na kuwasha taa zao kwa madereva wengine.

Kama dereva jauri anakuzuia au kufanya kitu kingine ambacho si salama, usijaribu kulipiza kisasi. Kuwa mtulivu. Waondokee madereva hawa. Usibishane nao. Kujaribu kulipiza kisasi na dereva jeuri ni wazo mbaya.

**Kushiriki barabara na Wanyama wa Kufugwa**

Mpanda mnyama anapokuwa anasafiri kwenye barabara kuu ya umma, au kuendesha gari linalovutwa na wanyama, hupewa haki zote za dereva wa gari. Itakuwa muhimu kwa dereva wa gari kupunguza kasi anapokabili hali kama hiyo, na labda hata kusimama, ili kufanya kila tahadhari inayofaa kuzuia hofu kwa mnyama/wanyama na kuhakikisha usalama na ulinzi wa mpanda mnyama/dereva. Dereva wa gari hapaswi kamwe kupiga honi yake au kuongeza mgurumo wa injini yake, hasa anapoendesha pikipiki, ili asishtue mnyama/wanyama wanapokutana, anapofuata au kupita wanyama kama hao. Tumia njia nzima ya magari ili kupita kabisa mnyama na kamwe usirudi kwenye njia yako haraka. Unapofuata farasi na mpanda farasi, farasi anayekokota kigari, au wanyama wanaochungwa, dumisha sekunde 4 za umbali wa kufuata. Dereva wa gari anaweza kutozwa faini au kufungwa kwa uendeshaji mbaya ya gari karibu na wanyama hao.



**Usalama wa Kongoni na Paa**

Mgongano na kongoni au paa unaweza kuwa mbaya sio kwa mnyama tu, lakini kwa dereva na abiria wa gari. Kundesha gari kwa tahadhari katika maeneo hayo kwenye barabara kuu yaliyo na alama za paa na kongoni wanaopita kunaweza kuokoa maisha na kuzuia majeraha. Uwepo wa kongoni na paa kwenye barabara kuu una uwezekano mkubwa wa kutokea wakati wa jioni, usiku na mapema asubuhi. Tumia tahadhari unapoendesha gari saa hizo wakati paa na kongoni huwa wanazurura au kulisha.



Mwanga kutoka kwa taa za mbele za gari unaweza kusababisha paa kusimama tuli kwa muda na kushindwa kuondokea gari, au inaweza kukimbia kwa kasi za hadi maili 40 kwa saa kuelekea mazingira yao. Hii ina maana kwamba kama paa yuko huo upande mwingine wa barabara kutoka mazingira yake, anaweza kugeuka na kukimbia mbele ya gari. Wanyama husafiri wawili-wawili, kwa hivyo uwe tayari kuona wa pili mara tu unapomwona wa kwanza.

Migongano na kongoni ni hatari zaidi kwa waendesha magari. Kongoni ni mzito zaidi kuliko paa—zaidi ya ratili elfu. Pia, wao ni warefu zaidi kuliko paa, na katika mgongano wanaweza kutua juu ya gari na abiria wake kwa nguvu ya kuponda. Macho ya paa huakisi taa za mbele. Kwa sababu kongoni ni warefu, macho yao hayawezi kuakisi taa za mbele za gari. Pia, kongoni ana rangi nyeusi zaidi kuliko paa. Sifa hizi hufanya iwe ngumu kuona kongoni katika masaa ya jioni.

## HALI HATARI ZA KUENDESHA GARI

**Mafuriko na Dhoruba**

Kitaifa, mafuriko ya ghafula husababisha vifo vingi kuliko tukio lolote la hali ya hewa. Karibu nusu ya vifo hivyo huhusiana na magari. Dhoruba, vimbunga vya theluji, na mifumo mingine ya hali mbaya ya hewa huleta hali hatarishi za kuendesha gari kama vile upepo mkali, kutoona vizuri, barabara telezi, na hatari zingine zisizotarajiwa. Wakati hali hatari za kuendeshea gari zinatabiriwa, ni bora kukaa nyumbani na kuepuka kusafiri zisizo za lazima. Hata hivyo, ukikumbana na dhoruba au hali ya hatari,

unapaswa kufanya yafuatayo:



- Punguza kasi yako. Usitumie kidhibiti mwendo. Kuwa macho.
- Dumisha zaidi ya sekunde nne za nafasi kati yako na gari lililo mbele yako.
- Kuwa macho hasa wakati wa usiku au unapoendesha gari kwenye barabar
- Fahamu kwamba madaraja, kalvati, na ukingo wa barabara zinaweza kubebwa na maji au kufukuliwa na maji ya mafuriko. Usiendeshe gari kuzunguka vizuizi vya barabara au kupita ishara za "barabara imefungwa". Tii ishara zote za mchepuo.
- Usiendeshe gari mahali ambapo maji yamefunika barabara. KKina cha maji sio dhahiri kila wakati na maji yanaweza kuficha hatari kama vile kuoshwa kwa barabara. Injini za magari zitazima ndani ya maji, na unaweza kusalia ukiwa umekwama au umebanwa.
- Kama gari lako litazima katika eneo lililofurika, achana nalo haraka iwezekanavyo. Maji ya mafuriko yanaweza kuongezeka kwa kasi na kubeba gari pamoja na abiria wake. Vifo vingi vimetokea kutokana na majaribio ya kusogeza magari yaliyokwama. Ukiamua kuacha gari lako katika eneo lililofurika, heshimu nguvu za maji yanayotiririka. Kiasi kidogo kama inchi 4 za maji kinaweza kusababishaa ugumu wa kutembea na kinaweza kuzuia hatari zisionekane.
- Upepo unaweza kuwa tatizo kwa madereva wote. Ni hatari hasa kwa magari makubwa na kwa madereva wanaovuta trela. Kuendesha gari kwa kasi ndogo ni utaratibu bora.
- Fahamu kwamba upepo mkali na theluji nzito au barafu zinaweza kusababisha miti na waya kuanguka kwenye barabara. Kamwe usikaribie au kuvuka waya zilizoangushwa.
- Angalia tahadhari za hali ya hewa na mafuriko ya ghafla zinazotolewa na Huduma ya Hali ya Hewa, pamoja na matangazo yote yanayohusu hali hatarishi za kuendesha gari.
- Wakati mwonekano ni hafifu, kama vile katika ukungu, mvua kubwa, au theluji nyingi, tumia taa zako za mbele za mwali wa mwanga mdogo. Ikiwa huwezi kuona wazi watu au magari futi 500 mbele, sheria inahitaji madereva kuwasha taa za mbele.

**Kuendesha gari Majira ya Baridi**

Majira ya baridi ni msimu mgumu zaidi wa kuendesha gari, kwa hiyo tumia tahadhari ya ziada. Hutakabiliana tu na theluji na barafu, lakini pia kuna masaa machache ya mwangaza wa mchana.

- Hakikisha kuwa breki zako, waipa za mbele, kiondoa ukungu, kikanza, na mfumo wa ekzosi viko katika hali bora.
- Kagua kishushamgando na uwe tayari kwa halijoto za baridi zaidi. Hakikisha tanki la maji ya kufuta kioo cha mbele limejazwa maji ya matumizi ya msimu wa baridi.
- Hakikisha una matairi mazuri ya wakati wa theluji kwenye magurudumu yote manne, na uyaweke mapema. Jaribu kutopatwa bila matairi hayo katika theluji ya kwanza. Kamwe usichanganye aina tofauti

ya matairi kwenye gari moja. Majimbo mengi huruhusu matairi yenye misumari ya chuma kutumika tu katika msimu wa baridi.. Daima hakikisha kuwa matairi yako yamejazwa hewa vizuri.

- Wakati wa dhoruba ya barafu au theluji, hasa wakati ushauri wa msafiri unatolewa, usiendeshe gari isipokuwa iwe ni lazima kabisa. Kama lazima uendeshe gari, ondoa kabisa barafu na theluji kutoka kwa gari lako lote na uhakikishe waipa za kioo cha mbele ziko hazina mkusanyiko wowote wa barafu. Ndani ya madirisha yako pia inapaswa kuwa bila unyevu.
- Wakati mvua ya mawe, mvua ya kuganda, au theluji inaanza kuanguka, barafu nyeusi inaweza kutunga haraka na huenda usiione. Madaraja, njia za kuingilia na kutoka, na madaraja ya juu zinaweza kuganda kwanza. Sehemu zenye utelezi zinaweza kubaki hata baada ya wafanyakazi wa barabara kusafisha barabara kuu.
- Kwa kuwa utahitaji kuendesha gari polepole zaidi, panga muda zaidi wa kufika unakoenda. Ongeza umbali wako wa kufuata hadi zaidi ya sekunde 4. Hata magari yenye magurudumu manne au yanayoendesha magurudumu yote hayana mshiko mzuri kwenye barafu. Magari yote yana ugumu wa kusimama, kupiga kona, na kubadilisha njia kwenye barabara za majira ya baridi.
- Kuwa mwangalifu hasa karibu na magari ya kufukua theluji—ni vigumu kuyaona kutokana na theluji inayorushwa nayo. Ni pana zaidi kuliko magari mengine, na mara nyingi husonga kwa mwendo wa polepole.
- Safiri mchana, usisafiri peke yako, na ufahamishe wengine kuhusu njia na ratiba yako. Kaa kwenye barabara kuu—epuka njia za mkato za vijijini.
- Kuwa tayari. Vitu ambavyo unapaswa kuweka kwenye gari lako ni pamoja na: Kuwa na kikwaruza kioo cha mbele na brashi, sepetu ndogo, mchanga wa paka au mchanga, nguo za ziada, chakula na maji, simu ya mkononi, maji ya ziada ya kuosha kioo cha mbele, vifaa vya msingi vya huduma ya kwanza, na tochi. Daima hakikisha una angalau nusu ya tanki la mafuta kwenye gari lako.

## Ukikumbwa na dhoruba ya theluji au ukikwama

- Toka kwenye barabara kuu. Washa taa za dharura na ubandike bendera ya dharura kwenye kipete cha mlango, antena, au dirisha.
- Baki kwenye gari lako ambalo waokoaji wanaweza kukupata kwa urahisi. Usitoke kwa miguu isipokuwa uone jengo karibu ambapo unajua unaweza kupata hifadhi. Kuwa mwangalifu: umbali hupotoshwa na upepo wa theluji. Jengo linaweza kuonekana karibu, lakini linaweza kuwa mbali sana kutembea kwa miguu kwenye theluji nene.
- Washa injini na kikanza kwa takriban dakika 10 kila saa ili ujipatie joto. Wakati injini imewashwa, fungua kidirisha chini kidogo ili hewa liingie. Ili kujilinda dhidi ya sumu ya kaboni monoksidi, hakikisha bomba la ekzosi halijazibwa na theluji.
- Fanya mazoezi ya mwili ili kudumisha joto la mwili, lakini usizidishe. Wakati wa baridi kali, tumia ramani, matandiko ya gari, na mikeka ya sakafu kama vifaa vya kuhifadhi joto. Kumbatana na abiria, na utumie koti lako kama blanketi.
- Laleni zamu tofauti. Mtu mmoja anapaswa kuwa macho wakati wote ili kusubiri vikundi vya uokoaji.
- Kunywa kinyuaji ili kuepuka upungufu wa maji mwilini. Hata hivyo, usinywe pombe.
- Kuwa mwangalifu usitumie vibaya nguvu za betri. Sawazisha matumizi ya umeme—kama vile taa, joto, na redio—na upatikanaji wake.
- Washa taa za ndani usiku ili wafanyakazi wa kazi au waokoaji waweze kukuona kwa urahisi.
- Ukikwama katika eneo la mbali, kanyaga kwa nguvu herufi kubwa katika eneo wazi, ukiandika HELP au SOS, na upange mawe au matawi ya miti ili kuvutia umakini wa wafanyakazi wa uokoaji ambao wanaweza kuwa wanatafuta eneo hilo kwa ndege.

## Kuteleza

Kuteleza kwa gari mara nyingi husababishwa na kushindwa kwa dereva kurekebisha kwa wakati kasi ya gari kulingana na hali ya barabara na magari. Hali hizi zinaweza kujumuisha theluji, barafu, mvua, udongo/changarawe, na majani yaliyo na unyevunyevu. Usitumie kidhibiti mwendo katika hali hizi. Katika gari lenye uendeshaji wa magurudumu ya nyuma, unaweza kuhisi kupoteza mshiko au mwanzo wa kuteleza. Hata hivyo, huenda kusiwe na onyo lolote kwenye gari lenye uendeshaji wa magurudumu ya mbele. Magari yenye uendeshaji wa magurudumu ya mbele yana udhibiti mzuri zaidi kwenye theluji, lakini hayana mshiko kamilifu, na utelezi waweza kutokea ghafla. Usiruhusu hisia nzuri na udhibiti wa gari lenye uendeshaji wa magurudumu ya mbele zikufanye uendeshe kwa kasi kuliko unavyopaswa.

## Jinsi ya Kuepuka Kuteleza.

Kwenye barabara ambazo zinaweza kuwa na utelezi, unapaswa kuendesha kwa kasi ya chini. Usibadilishe kasi au mwelekeo ghafla . Ili kupunguza kasi kwenye barabara telezi, unapaswa kuondoa mguu wako kwenye kichapuzi ili kupunguza kasi na kusaidia udhibiti wa gari lako. Kama unahitaji kupunguza kasi zaidi, "bana" kwa upole breki zako kwa shinikizo la polepole na la taratibu. Ruhusu magurudumu yaendelee kuzunguka. Kama yataanza kukwama, legeza mguu wako kwenye kanyagio la breki kwa upole. Unapopunguza kasi, inaweza pia kusaidia kubadilisha gia na kuingia kwenye gia ya chini. Ikiwa gari lako limewekewa breki za kuzuia kukwama, tumia shinikizo la breki kwa uthabiti, usisukume breki mara kwa mara! Fuata maelekezo kwenye mwongozo wa mmiliki wa gari lako.

## Jinsi ya kudhibiti gari katika Utelezi

Njia bora ya kurejea kutoka kwenye utelezi ni sawa kwa magari yote ya magurudumu ya mbele na ya nyuma:

- Usikanyage breki, itafanya utelezi kuwa mbaya zaidi.
- Geuza usukani kuelekea upande unaotaka gari liende.
- Huenda ukahitaji kugeuza usukani kushoto na kulia mara kadhaa ili kudhibiti kabisa gari lako.



**KUMBUKA:** Uboreshaji wa gari, kama vile imarisho la udhibiti, unaweza pia kukusaidia kudhibiti gari lako, lakini hauwezi kuwa mbadala wa tahadhari ya dereva. Magari yanayoendeshwa kwa magurudumu manne na yale ya magurudumu yote yana mshiko bora zaidi kwenye theluji, lakini sio kwenye barafu. Jihadhari kujiamini kupita kiasi unapoyatumia magari haya.

Haijalishi ni aina gani ya gari unalo, ni wazo nzuri kwenda kwenye uwanja wa maegesho usio na watu na kujifunza jinsi gari lako linavyokabili barabara zenye barafu au theluji.

## Breki za Kuzuia Kukwama

Breki za kuzuia kukwama ni uvumbuzi muhimu katika usalama. Hukuruhusu kufunga breki na kudhibiti gari kwa wakati mmoja. Tarajia kelele na mtetemo katika kanyagio la breki. Usikanyagekanyage

breki au kuondoa mguu kwenye kanyagio la breki kwa sababu itawachilia mfumo wa breki za kuzuia kukwama.

Mwongozo wako wa mmiliki utakuambia kama gari lako lina ABS. Pia, taa la onyo la ABS litaonyeshwa kwa muda mfupi kwenye dashibodii yako unapogurumisha gari lako.

**Kumbuka:** Ikiwa taa yako ya ABS itaendelea kuwaka baada ya kuanza kuendesha gari, mfumo wa ABS wa gari lako haufanyi kazi. Hata hivyo, gari bado lina breki .

**Mwonekano Uliopungua**

**Kuendesha Gari Mchana**

Utafiti umeonyesha kuwa kuendesha gari taa za mbele zikiwa zimewashwa kwa mwali wa mwanga mdogo wakati wa mchana hupunguza hatari ya kugongana ana kwa ana kwa zaidi ya 20%. Watengenezaji wa magari wameweka taa za mchana kwenye magari mengi. Hizi taa hujiwasha na hazipaswi kuchanganywa na taa za mbele za kawaida. Taa za mchana na taa za mbele zinaweza kusaidia madereva wengine kuona gari lako wakati wa mchana. Kumbuka, wakati theluji, mvua, na ukungu vinapunguza mwonekano unapaswa kuwasha taa zako za mbele. Mazoea bora ni kuendesha gari ukiwa umewasha taa zako za mbele za mwali wa mwanga ukiwa chini, hata wakati wa mchana.

## Kumbuka: Taa za maegesho zinapaswa kutumika tu wakati gari lako limeegeshwa.

**Kuendesha Gari Usiku**

Ni hatari zaidi kuendesha gari usiku kuliko mchana kwa sababu huwezi kuona mbali usiku. Sheria inahitaji taa za mbele za magari kuwashwa nusu saa baada ya machweo hadi nusu saa kabla ya macheo. Hakikisha umewasha taa zako za mbele—taa zako za mchana zinazowaka zinaweza kukupa hisia kwamba taa zako za mbele zimewashwa.

Daima unahitaji kuona sekunde 4 mbele. Unapoendesha gari usiku kwa mwendo wa maili 40 kwa saa, ukiwa na taa za mbele zenye mwali wa mwanga mdogo, huwa "unazichosha taa zako za mbele." Hii inamaanisha kuwa huwezi kuona mbali vya kutosha ili kusimama katika nafasi unayoiona, na huenda usiweze kukwepa mgongano.

**TUMIA TAA ZA MWALI WA MWANGA ZA JUU NA ZA CHINI IPASAVYO**

Tumia mwali wa mwanga wa juu unapoendesha gari maeneo ya vijijini yenye magari machache. Hata ukiwa na mwali wa mwanga wa juu, kasi lazima iwe ya chini zaidi kuliko wakati wa mchana.

Daima tumia mwali wa mwanga wa chini unapokaribia magari mengine au watembea kwa miguu ili usimtie kiwi dereva au mtembea kwa miguu. Pia tumia mwali wa mwanga wa chini unapoendesha gari katika maeneo yenye taa za barabarani au ukungu na unapoifuata gari lingine.

**Madereva Wenye Heshima Hufifiliza Taa Zao za Mbele**

Unapoendesha gari usiku, unapaswa kufifiliza taa zako za mbele wakati unapokutana na au kufuata gari lingine

**Kukaribia Taa za mbele**

Ukiangalia moja kwa moja taa zinazokuja, unaweza kutiwa kiwi kwa sekunde kadhaa. Ili kuepuka kutiwa kiwi kwa muda, unapaswa kuangalia mbele kuelekea ukingo wa kulia wa

barabara kuu hadi taa angavu zipite na uwezo wako wa kuona umerudi kawaida. Mazoea haya pia yatakusaidia kugundua waendesha baiskeli au watembea kwa miguu wanaoweza kuwa karibu na ukingo wa barabara.

## KUENDESHA GARI KWENYE BARABARA KUU ZA JIMBO

Barabara kuu za jimbo ni barabara za njia nyingi zilizogawanywa, ambazo zimeundwa kwa ajili ya mwendo wa kasi. Katika maeneo mbalimbali, zinajulikana kama barabara za mwendo kasi, baraste, barabara za ushuru, barabara za kulipia kodi, barabara za upatikanaji haba au barabara kuu. Baadhi ya barabara hizi ni za bure, na zingine zinahitaji kulipiwa ushuru.

Zote zina faida kadhaa muhimu. Hizi ni barabara zenye njia nyingi na ufikio unaodhibitiwa, ambapo unaweza kuendesha gari kwa umbali mrefu bila usumbufu. Barabara hizi zimeundwa kwa ajili ya usafiri wa haraka na salama. Ni muhimu ujifunze kutumia barabara hizi ipasavyo.

**<u>Njia za Kubadilisha Kasi (Kuharakisha na Kupunguza Kasi).</u>**

Kuna njia zinazoambatana na barabara kuu za jimbo kwa umbali mfupi, ambazo zinaunganisha barabara za kuingia au kutoka kwenye barabara kuu ya jimbo. zimeundwa ili magari yaweze kuongeza au kupunguza kasi wa wa kuingia au kutoka kwenye njia za magari.




**<u>Njia za Kuingia</u>**

Hii ni barabara fupi ya njia moja inayoelekea kwenye barabara kuu ya jimbo. Unahitaji kuangalia kwa makini ili kuingia kwenye magari yanayosonga kwa kasi. Njia ya kuingia hukupeleka kwenye njia ya kuongeza kasi ambapo magari huendeshwa kwa kasi ya barabara kuu ya jimbo. Kaa kulia, toa ishara kushoto, weka kasi, angalia eneo fiche upande wa kushoto na ufanye mabadiliko ya njia wakati njia ya kusafiria ni salama. Dereva anayeingia lazima awapishe madereva ambao tayari wapo kwenye barabara kuu ya jimbo.

**<u>Njia ya Kutoka</u>**

Hii ni barabara fupi ya njia moja inayounganisha barabara kuu ya jimbo na barabara nyingine na hukuwezesha utoke kwa kasi salama. Unapotoka barabara k unapaswa kutoa ishara ya kubadilisha njia, uingie kwenye njia ya kupunguza kasi iliyo karibu sana na sehemu ya kutoka, na upunguze kasi hadi ile iliyowekwa.




**<u>Kuendesha Gari Salama kwenye Barabara za kuu za jimbo</u>**

1. Endelea kupekua ili kujua kinachoendelea karibu nawe, na uangalie vioo vyako mara kwa mara.
2. Usilikaribie sana gari linalokutangulia. Njia rahisi ya kujua kama uko umbali salama kutoka kwa gari lililo mbele yako ni kutumia sheria ya umbali wa sekunde 4. Ikiwa barabara ina unyevu au ni telezi, utahitaji nafasi ya ziada.
3. Julisha madereva wengine unachokusudia kufanya kabla ya kukifanya. Kamwe usipunguze kasi au kubadilisha njia ghafla. Mabadiliko ya mara kwa mara ya njia si salama.
4. Kabla ya kubadilisha njia au kupita, angalia vioo vyako, toa ishara, na uangalie maeneo fiche katika mwelekeo ambao unakusudia kwenda.

5. Kamwe usisimame kwenye njia ya magari. Ni kinyume cha sheria kusimama kwenye barabara ya kuu ya jimbo isipokuwa wakati wa dharura. Kama ni lazima usimame kwa dharura, ingia kwenye njia ya dharura na uweke gari mbali kulia iwezekanavyo. Kama unahitaji msaada, inua boneti ya gari lako, funga kitambaa cheupe kwenye gari, na ubaki ndani ya gari lako.
6. Unapaswa kuendeshea gari kwenye njia ya kulia isipokuwa unapolipita gari lingine au kama ishara inaonyesha vinginevyo.
7. Usiendeshe gari wakati umechoka. Kuendesha gari ukiwa umechoka ndio sababu kuu ya ajali kwenye barabara kuu za jimbo. Kama umechoka, ni muhimu usimame na kupumzika katika eneo salama haraka iwezekanavyo.
8. Barabara kuu za jimbo zenye barafu na theluji pamoja na njia zake za kuingia na kutoka zinaweza kuwa hatari sana. Kumbuka kupunguza kasi na kuendesha gari kwa uangalifu. Pia, madaraja na madaraja yapitayo juu ya barabara yanaweza kuteleza kuliko barabara kuu.
9. Ikiwa umepita njia yako ya kutoka, usisimame na kurudi na kamwe usitumie mzunguko wa dharura. Vivuko hizi ni za magari ya dharura na ya matengenezo tu. Endelea hadi kwenye njia ya kutoka inayofuata.
10. Kamwe usitumie kidhibiti mwendo katika hali za kuendesha gari kama vile mvua, ukungu, theluji, barafu, n.k.
11. Unapokaribia gari lolote la kutekeleza sheria, la dharura, au la matengenezo ambalo taa zake zinamweka pembeni mwa barabara, punguza mwendo. Sheria inasema lazima uendelee kwa tahadhari na ubadilishe njia mbali na gari la dharura mara tu inapokuwa salama kufanya hivyo. Ikiwa huwezi kubadilisha njia lazima upunguze kasi hadi maili 20 kwa saa chini ya kikomo cha kasi ili kuyapita magari yaliyosimamishwa.

Inamaanisha nini ikiwa, unapoendesha gari kwenye barabara kuu iliyogawanywa, ukingo wa barabara upande wa kulia umechorwa rangi ya manjano? Unakwenda NJIA ISIYO SAHIHI kwenye barabara kuu iliyogawanywa au barabara kuu ya jimbo. Kwenye barabara kuu iliyogawanywa, mstari wa upande wako wa kulia unapaswa kuwa mweupe.




**KUPITA**

Unapokaribia gari lingine au baiskeli kutoka nyuma na unataka kupita, hakikisha una umbali wa kutosha kupita salama. Toa ishara ya kushoto ili kujulisha madereva wengine kuwa utatoka, angalia nyuma ili kuona ikiwa gari lako linapitwa (angalia kwenye vioo vya nyuma na upande wako wa kushoto kukagua eneo fiche), badilisha njia na upite upande wa kushoto. Usiku, inaweza kuwa muhimu kupepesa taa zako kutoka mwanga hafifu hadi mkali na hafifu tena ili kumwonya dereva aliye mbele yako kwamba unakusudia kupita.

Ikiwa unapita huku ukivuta trela, kuwa makini hasa kwamba umepita ifaavyo gari au baiskeli unayopita kabla ya kurudi kwenye njia yako ya usafiri.

Unapovuta mzigo mpana au kuendesha gari lenye upana kuliko kawaida, kuwa makini sana unapopita gari lingine lolote au mwendesha baiskeli.

Pita magari na baiskeli upande wa kushoto. Acha angalau urefu wa futi nne kati ya gari lako na gari au baiskeli yoyote unayopita. Unapaswa kwenda mbali ya kutosha mbele ya gari au baiskeli unayopita ili uweze kuona sehemu yote ya mbele ya gari au mwendesha baiskeli ndani ya kioo cha nyuma. Tumia ishara yako ya kulia, angalia eneo fiche la kulia juu ya bega lako, na urudi upande wa kulia wa barabara. Unapopitwa na gari lingine, unapaswa kupunguza kasi kidogo na kubaki upande wa kulia. Hii itamruhusu yule dereva mwingine kupita kwa usalama zaidi.

Dereva anaweza kupitia upande wa kulia mwa gari lingine kwenye barabara yenye njia nyingi. Kwenye barabara zisizo za njia nyingi, dereva anaweza kupitia upande wa kulia wa gari au baiskeli inayogeuka au inayojiandaa kugeuka kushoto, ikiwa kuna nafasi ya kupita kwa salama. Hakuna hali yoyote inayoruhusu gari kupitwa kwa kuendesha nje ya lami au sehemu kuu ya barabara inayotumika.

## USIPITIE MAENEO HAYA




- Vilima
- Kona
- Njia ya reli
- Makutano
- Ukiona "njia iliyobadilika mbele"

## KUENDESHA GARI KAMA UMEDHURIKA

Ingawa madereva wengi hufikiria tu pombe wanaposikia neno kudhurika, kunywa pombe sio njia pekee ambayo dereva anaweza kuwa amedhurika. Dawa, hata zile za maelekezo ya daktari na zile za kununua bila agizo, zinaweza kuathiri sana uwezo wako wa kuendesha gari kwa salama. Kuendesha gari huku ukisinzia kunaweza pia kuathiri uwezo wako wa kuendesha gari na kunaweza kuwa hatari sana.

**<u>Pombe na dawa zingine</u>**

Dereva anayekunywa pombe ndiye sababu kuu ya ajali mbaya za barabarani. Kwa wastani, mtu mmoja huuawa na dereva mlevi kila baada ya dakika 40.

Ni kinyume cha sheria kuendesha gari ukiwa umekunywa pombe au kutumia dawa zingine. Madereva waliokunywa pombe au kutumia dawa zingine hawana udhibiti mzuri juu yao wenyewe au wa gari, na huhatarisha maisha yao wenyewe na ya wengine. Sheria ya Vermont inasema kwamba wakati mkusanyiko wa pombe kwa damu ya mtu (BAC) ni .08 au zaidi, yuko "chini ya ushawishi" au "amedhurika". Ni muhimu kukumbuka kwamba viwango vya mtu kudhurika ni mkusanyiko wa pombe kwenye damu wa chini ya .08. Hata kinywaji kimoja huharibu uamuzi wako.

Watu walio chini ya umri wa miaka 21 wanaoendesha gari wakiwa na mkusanyiko wa pombe wa .02 au zaidi wanaweza kupatwa na ukiukaji wa sheria za trafiki. Leseni ya Dereva itasimamishwa, na dereva atalazimika kukamilisha programu ya elimu ya pombe na uendeshaji kwa gharama zake mwenyewe.

**Pombe Huathirije Ujuzi Wako wa Kuendesha Gari?**

Pombe ni dawa; inaweza na itaathiri uendeshaji wako. Pombe ikinywewa, maamuzi unayofanya yanaweza kuwa yenye makosa. Pombe inaweza kuonekana kama inakupa msisimko; haifanyi hivyo. Huathiri mchakato wako wa mawazo. Pombe, kwa kweli, ni kipozo; Itakuathiri kwa njia zifuatazo:

- **Uamuzi**- Huenda usiwe na uwezo wa kufanya maamuzi mazuri kuhusu uendeshaji gari. Huenda ukafikiri uko sawa, lakini hujui hatari unazoweza kuwa unachukua.
- **Uwezo wa kuona** - Uwezo wako wa kuona wa jumla unaweza kupungua kwa kiasi kikubwa.
- **Umakinifu** - Akili yako hutangatanga, na huwezi kumakinika.
- **Uelewa** - Kiwango chako cha ufahamu kuhusu yanayotokea karibu nawe kitadhoofika. Huenda usitambue unachokifanya.
- **Hisia (Akili)** - Hisia zako hukandamizwa; huhisi mwendo hivyo hutaelewa kuwa unaweza kuwa unazidisha mwendo.
- **Muda wa kuchukua hatua** - Itakuchukua muda mrefu zaidi kuchukua hatua na kusogeza mguu wako kutoka kwenye kichapuzi hadi kwenye breki. Muda huu wa kuchukua hatua pole pole unaweza kuwa tofauti kati ya kufika salama au kutofika kabisa.

Muda ndio njia pekee ya kupunguza athari za pombe. Kukunywa kahawa, kuoga na maji baridi au kukimbia hakutamfanya mtu kutoa ulevi haraka. Huchukua angalau saa moja kwa kila kinywaji ili pombe na athari zake kusafishwa mwilini mwako. Hii ina maana kwamba unaweza kusubiri saa kadhaa ili kupunguza madhara ya pombe ili uweze kuendesha gari kwa usalama.

**Dawa Zingine**

Kuendesha gari baada ya kutumia dawa zingine au dawa za kulevya (hata zile za maelekezo na za kununua bila ya agizo) kunaweza kuwa hatari kama pombe, hata zaidi kwa baadhi ya watu. Dawa zinaweza kukufanya uwe na usingizi na kukufanya ushindwe kufikiri au kutenda ipasavyo. Kuhisi hivi unapoendesha gari kunaweza kukupeleka kwenye mauti barabarani. Tena, muda ndio njia pekee ya kupunguza athari za dawa yoyote.

Ukipatikana na hatia ya DUI au kuendesha gari baada ya kutumia dawa, leseni yako itasimamishwa. Lazima ulipe faini kubwa, ada ya wakili, ugharamie darasa la elimu ya pombe, unaweza kwenda jela na bima yako itaongezeka.

Vermont ina Sheria ya "Idhini Iliodokezwa" - Hii ina maana kwamba mtu anapopata leseni, mtu huyo anakubali kusema "ndiyo" anapoombwa kufanya kipimo ili kuona kiasi cha pombe au dawa nyingine ziko mwilini mwake. Afisa wa polisi anaweza kuomba dereva kufanya kipimo kama afisa anadhani dereva ameathirika na pombe au dawa zingine. Dereva akikataa, atanyanganywa Leseni ya Dereva kwa angalau miezi sita (6).

**KUMBUKA:** Vermont ina mchakato wa kusimamisha leseni kiutawala, ambayo ina maana kwamba unaweza kupoteza leseni yako kupitia mchakato wa kiraia kabla ya hukumu ya uhalifu ya DUI.

## FIKIRIA KABLA YA KUNYWA POMBE!

Kama unapanga kunywa, fanya mipango kabla ya kuanza

- Tumia dereva aliyeteuliwa na uhakikishe kuwa dereva hanywi pombe. Dereva aliyeteuliwa hukubali kutokunywa pombe au kutumia dawa zingine, na ana jukumu la kurudisha wengine nyumbani wakiwa salama.
- Mpigie simu mzazi, au mtu mwingine anayewajibika ili kupanga safari salama ya nyumbani.

- Panga kulala ulipo, ikiwa ni salama kufanya hivyo.
- Sikiliza marafiki zako. Wakikuonya kutoendesha gari, chukulia wasiwasi wao kwa umakini.
- Kabla ya uanze kunywa, mpe rafiki ambaye hanywi funguo za gari lako, na ambaye hatakuruhusu kuendesha gari kama umekunywa.

Muda ndio njia pekee ya kupunguza athari za pombe. Inachukua angalau saa moja kwa kila kinywaji cha pombe na athari zake kutolewa nje ya mwili wako. Hii ina maana kuwa huenda ukasubiri saa kadhaa ili kupunguza athari za pombe ili uweze kuendesha gari kwa usalama. Kukunywa kahawa, kuoga, kufanya mazoezi, nk, haziwezi kupunguza BAC yako au madhara ya pombe.




Chama cha Wauguzi wa Dharura cha Vermont (ENCARE) hufadhili uwekaji wa mabango kwenye maeneo ya ajali mbaya za barabarani zinazohusiana na pombe. Unapoona mojawapo ya ishara hizi, inamaanisha mtu alikufa katika eneo hilo kwa sababu ya dereva mlevi.

Kama unasikitishwa na unywaji wako, wasiliana na VT Helplink. VT Helplink ni huduma ya bure na ya siri ya msaada na uelekezi kuhusu pombe na madawa ya kulevya inayotolewa na Idara ya Afya ya Vermont. Mtaalamu anayejali na aliyefunzwa atakusaidia wewe au mpendwa wako kuchukua hatua kwa ajili ya kupona.

Tembelea VTHelplink.org au upige simu 802-565-LINK (au simu ya bila malipo 833-565-LINK)

**Kuendesha Gari Ukiwa na Usingizi**

Kila mwaka, ajali nyingi hutokea kwa sababu dereva hulala usukani. Hii inaweza kusababisha ajali mbaya ya kugongana uso kwa uso na gari lingine, mti, au kitu kingine cha pembeni mwa barabara. Madereva walio na usingizi wanaweza kuendesha gari vibaya kiasi kwamba wanaweza kuonekana kuwa walevi.

Baadhi ya dalili za kuendesha gari ukiwa na usingizi ni:

- Kuwa na matatizo ya kuzingatia au kuweka macho yako wazi
- Kupiga miayo mara kwa mara
- Kutokumbuka maili chache ulizopita mwisho ukiendesha gari
- Kutangatanga kutoka njia ya kusafiri
- Kutoziona ishara za barabara

Watu walio katika hatari kubwa ya kupata usingizi wakiendesha gari ni wale huendesha baada ya kukosa usingizi wa kutosha. Mara nyingi hii ni pamoja na vijana, wafanyakazi wa zamu na watu wanaofanya kazi muda mrefu sana. Pia inajumuisha watu ambao wanaweza au hawawezi kutambua kuwa wana ugonjwa wa usingizi. Madereva wanaweza kujua wamechoka lakini waamini wanaweza kukaa macho. Kwa bahati mbaya, badala ya kukaa macho wanaweza kulala na kusababisha ajali.

Epuka kuendesha gari ukiwa na usingizi. Ukianza kusinzia ukiwa barabarani, tafuta mahali salama pa kuegesha na kusimama. Kufungua dirisha lako na kuwasha redio yako hakutazuia kulala. Kwa kweli, unapoanza kutafuta njia ya kukaa macho, hiyo ni dalili ya uhakika kuwa unahitaji kusimama na kupumzika.

## KUENDESHA GARI UKIWA NA MVUTO WA MAWAZO

Uchunguzi unaonyesha kuwa chochote kinachoondoa umakini wako kutoka kwa kuendesha gari kinaweza kusababisha ajali.

Haijalishi ni nini kinavuta mawazo, madereva ambao huvutwa mawazo huonyesha aina sawa ya tabia ya msingi. Mivuto ya mawazo hufanya madereva kuchukua hatua polepole zaidi katika hali ya trafiki au matukio, kama vile kusimamisha gari ili kuingia kushoto au kujiondoa kutoka barabara ya pembeni.

Madereva walio na mvuto wa mawazo hushindwa mara nyingi kutambua hatari zinazoweza kutokea kama vile watembea kwa miguu, waendesha baiskeli au vifusi barabarani. Madereva walio na mvuto wa mawazo pia hupunguza "nafasi ya usalama", na kufanya jambo la hatari ambalo vinginevyo hawangefanya, kama vile kugeuka kushoto mbele ya trafiki inayokuja. Kutokuwa makini na kukosa kupisha mwingine ni vitendo vya kawaida vya madereva vinavyosababisha ajali za magari na watembea kwa miguu au waendesha baiskeli huko Vermont.

## Kukabiliana na Mivuto ya Mawazo

- Panga mapema vituo vyako vya redio unavyopenda ili kuvifikia kwa urahisi na upunguze vya kutosha sauti ya redio yako ili uweze kusikia sauti za nje ya gari lako, kama vile king'ora, honi, au mlio wa treni.
- Mteue abiria wa kiti cha mbele kuwa "msaidizi wa dereva" badala ya kuhangaika na ramani au mifumo ya urambazaji. Iwapo unaendesha gari peke yako, panga njia na mahali unapokwenda mapema.
- Epuka kula na kunywa unapoendesha gari. Hakikisha vyakula vyote vimewekwa vizuri na vinywaji vimewekwa salama kwenye vibebea vikombe.
- Usipuuze jinsi watoto wanavyoweza kukuvuruga ndani ya gari. Wafundishe umuhimu wa tabia njema wakiwa ndani ya gari.
- Pumzika ikiwa utajikuta "umepotea katika mawazo" unapoendesha gari.
- Kumbuka kuzingatia kuendesha gari na kuepuka kuvutwa mawazo na watu au vitu ndani na nje ya gari lako.
- Fanya maandalizi yako binafsi nyumbani, siyo ndani ya gari.
- Wanyama wa kipenzi wanaweza kuvuruga umakini, hivyo wanapaswa kuwa ndani ya kibebea, sio kwenye mapaja yako au wakitembea huru.
- Kuvuta sigara ni mvuto ya mawazo. Epuka kuvuta sigara unapendesha gari.

## Kukabiliana na Hisia

Hisia huathiri kuendesha gari kwa usalama. Huenda usiweze kuendesha gari vizuri ukiwa na wasiwasi mwingi, msisimko, hofu, hasira au huzuni.

Jipe muda wa kutulia na kupoa. Kutembea ni njia nzuri ya kufanya hivyo.

Panga kimbele. Jipe muda wa ziada kwa safari yako ya kuendesha gari. Ondoka dakika chache mapema. Kama una muda mwingi, kuna uwezekano mdogo wa kuharakisha, kuvunja sheria au kusababisha ajali.

## Simu za Mkononi na Vifaa Vingine vya Elektroniki

- Ni kinyume cha sheria kwa madereva kusoma au kutuma jumbe wanapoendesha gari.
- Ni kinyume cha sheria kwa madereva kutumia kifaa cha elektroniki kinachobebeka wanapoendesha gari kwenye barabara kuu ya umma huko Vermont, ikiwa ni pamoja na wakati gari limesimama
- Mtu atakayekiuka sheria hii atatozwa faini isiyopungua dola $100.00 na isiyozidi $200.00 kwa kosa la kwanza, na isiyopungua $250.00 wala kuzidi $500.00 kwa ukiukaji wa pili au wa baadae.
- Mtu anayepatikana na hatia ya kuvunja kifungu hiki wakati wa kuendesha gari ndani ya eneo la kazi lililoainishwa vizuri ambako kuna wafanyakazi wa ujenzi, matengenezo, au huduma za umma, atatolewa pointi mbili kwenye rekodi yake ya udereva kwa kosa la kwanza na pointi tano kwa kosa la pili au la baadaye.
- Tambua kuwa kuendesha gari kunahitaji umakini wako kamili.
- Kama unahitaji kupiga simu, muulize abiria kwenye gari apige simu au usimame mahali salama kabla ya kupiga simu yako.

- Usiijibu simu yako ya mkononi. Mruhusu mpigaji simu aache ujumbe, na umpigie simu baadaye unaposimama katika eneo salama.
- Weka simu yako ndani ya gari ili isije ikawa kifaa cha hatari wakati wa ajali.

## JARIBIO (LA UJUZI) WA BARABARA

Unapofanya jaribio la leseni ya barabarani, mtahini ataangalia ili kuona kama unaweza kuendesha gari kwa usalama, kwa heshima na kwa usahihi. Lazima pia uonyeshe kuwa unaelewa na unaweza kufuata sheria za barabara.

### Kusimama na Kuanzisha Gari kwenye Kilima

Unapofanya jaribio lako la barabarani, mtahini atakwambia usimamishe na uanzishe gari kwenye kilima. Utaagizwa kuendeshea gari upande wa kulia wa barabara, kusimama, kisha kuweka breki ya maegesho/breki ya dharura na kuweka gia huru. Hakikisha kuweka ishara ya kulia kuwaambia wengine unachokifanya. Breki ya maegesho/breki ya dharura inapaswa kuzuia gari lisirudi nyuma.

Kabla ya kupanda mlima, weka gari kwenye gia. Weka ishara ya kushoto. Angalia vioo vyako, na eneo fiche la kushoto kuhakikisha hakuna magari. Ongeza kasi kwa utaratibu hadi uhisi gari linataka kuanza kusonga na kisha uachilie breki ya kuegesha ili kuzuia kurudi nyuma, na uangalia tena juu ya bega lako la kushoto kabla ya kuondoka. Unapaswa kuweza kuendesha gari juu ya kilima bila kurudi nyuma.

**KUMBUKA:** Unaweza kuhitaji kusimama kwenye kilima kwa ishara ya kusimama, taa ya trafiki, au dharura kama mbwa anayeingia barabarani. Ili kuzuia kurudi nyuma wakati wa kuanzisha gari kwenye kilima, dereva anaweza kutumia mojawapo ya mbinu hizi zifuatazo:

- Ondoa mguu wako haraka kutoka kwa breki hadi kwa kichapuzi.
- Weka breki yako ya maegesho/dharura. Weka mguu wako wa kulia kwenye kichapuzi. Kanyaga kichapuzi polepole na kwa utaratibu kisha achilia breki ya maegesho/dharura ili kuendelea na kilima.

**KUMBUKA:** Unapoendesha gari kwa mteremko, hupaswi kuteremka mlima klachi ikiwa chini au gia ikiwa huru.

### Kugeuka

Unapofanya mtihani wako wa kuendesha gari, utahitajika kuonyesha utaratibu ufuatao wa kugeuka, kwa kutumia barabara ya kando.

1. Unapokaribia barabara ya kando upande wa kulia kama ulivyoagizwa na mtahini, punguza kasi na uangalie magari pande zote. Washa taa yako ya mwelekeo ili madereva wengine wajue unachofanya.
   Endesha gari kidogo kupita barabara na usimame takriban inchi 18 kutoka kwenye ukingo wa barabara. Weka gia ya nyuma. Angalia magari pande zote kabla ya kurudi nyuma. Kumbuka kupekua maeneo yako fiche .




2. Wakati njia ya kando iko wazi, rudi polepole ndani yake. Kuwa mwangalifu na ukae upande wako wa barabara. Angalia hasa kupitia dirisha la nyuma wakati wa kurudi nyuma. Acha kurudi nyuma gari lako likiwa limeingia kikamilifu kwenye barabara ya kando, mbele ya njia za watembea kwa miguu au mistari ya kusimama.

3. Kabla ya kurudi barabarani, washa ishara ya kushoto na uweke gia ya kuendesha. Kama hakuna magari yanayokuja, geuka kwa usahihi kuelekea kushoto ili kumaliza mzunguko.

Daima angalia nyuma yako na urudishe gari polepole. Kamwe usirudi nyuma kwenye makutano. Kumbuka, unaporudisha gari lako nyuma, unawajibika kwa magari katika pande zote!

**Kumbuka:** Kuna chaguzi zingine kadhaa za kugeuza gari lako. Chaguo unalofanya linategemea hali ya trafiki na kama ni halali au la. Kuzunguka mtaa au kutumia sehemu ya maegesho ni chaguo salama zaidi.

## Maegesho ya Sambamba

Pia utahitajika kuegesha sambamba wakati wa jaribio lako la barabara.

### Kuingia Eneo la Maegesho

Wakati wa kukaribia eneo la maegesho, angalia kioo chako cha nyuma na uweke ishara kulia. Simama kando ya gari la mbele, umbali wa futi mbili hadi tatu. Weka gia ya nyuma. Angalia magari na watembea kwa miguu pande zote kabla ya kurudi nyuma. Angalia juu ya bega lako la kushoto ili kuangalia maeneo fiche.

Ukitumia picha zilizo hapa chini kama mwongozo, peleka gari lako kwenye nafasi. Kuna njia kadhaa za kufanikisha hili. Njia zote zinahitaji kugeuza usukani kikamilifu kutoka kulia hadi kushoto na kuangalia kupitia dirisha la nyuma wakati wa kurudi polepole. Polepole songa mbele ili kuweka gari katikati ya nafasi.




### Kuondoka Kwenye Maegesho

Kama ni lazima, rudisha gari kwenye nafasi ambayo kuingia tena kwenye njia ya magari kunaweza kufanywa kwa mwendo mmoja. Toa ishara ya kushoto, angalia kote kwa magari yoyote, waendesha baiskeli na watembea kwa miguu (angalia vioo vya kukagua nyuma na vya upande, na uangalie bega lako la kushoto kwenye eneo fiche). Kama hakuna magari, ondoka kwa uangalifu. Ingia barabara polepole, ukihakikisha umekaa upande wako.

**Kumbuka:** Katika jaribio la barabarani, unaweza kuhitajika kuegesha sambamba na gari la mbele linalopatikana tu. Hakikisha bado unafuata taratibu zizo hizo.

## AJALI

Maamuzi mabaya yanayofanywa na madereva husababisha ajali nyingi. Baadhi ya mifano ni:

1. Kuendesha gari haraka zaidi dhidi ya hali Za barabara.
2. Kutokuwa makini na uendeshaji wao.
3. Kuendesha gari karibu sana na gari lililo mbele yao.
4. Kuendesha gari juu ya mstari wa kati.
5. Kutotoa haki ya kupita.
6. Kuendesha gari baada ya kunywa pombe au kutumia dawa zingine.
7. Kupita wakati si salama kufanya hivyo.
8. Kutoangalia vioo na maeneo fiche.

### Cha Kufanya Baada ya Ajali

Dereva ambaye amehusika katika ajali anahitajika na sheria kusimama na kutoa msaada wowote ambao ni muhimu. Mara nyingi wanaohusika katika matukio ya ajali huchanganyikiwa na kukasirika, kwa hivyo jitayarishe kwa hali za ajali. Ni muhimu kufikiria hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika eneo la ajali.

1. Ikiwezekana, sogeza magari yaliyohusika kutoka kwenye njia za magari na kuyaweka pembezoni mwa barabara. Hii itapunguza uwezekano wa mtu mwingine kugonga magari yanayohusika, na kusababisha uharibifu na majeraha zaidi.
2. Kama mtu amejeruhiwa, piga simu 911. Mwache majeruhi mahali alipo. Unaweza kumdhuru majeruhi zaidi kwa kumwondoa kwa njia isiyo sahihi. Mtulize na umpe joto majeruhi
3. Afisa wa polisi atajibu simu ya 911 na kuangalia eneo la ajali. Afisa wa polisi anaweza kupata ukweli kuhusu nini kilichotokea. Polisi hawatapendelea upande wa dereva huyu au yule. Utalazimika kumwonyesha afisa wa polisi leseni yako, thibitisho la usajili halali na bima. Lazima pia uonyeshe leseni yako kwa mtu yeyote aliyejeruhiwa au ambaye mali yake imeharibiwa.




4. Ukigonga gari lililoegeshwa na kusababisha uharibifu, na huwezi kumpata mmiliki, lazima uandike jina lako, anwani na nambari ya simu na kuziacha ndani, au juu ya gari. Hii itamwezesha mmiliki kujua ni nani wa kuwasiliana naye.
5. Kama mtu yeyote amejeruhiwa, au kama uharibifu ni zaidi ya $3,000, lazima utoe ripoti ya maandishi kwa Idara ya Magari ndani ya masaa 72. Ripoti za ajali husaidia jimbo kuboresha barabara.

### Ripoti za Ajali

Unaweza kupata Ripoti ya Ajali ya Vermont katika Idara yoyote ya Polisi ya Vermont au kwa kuwasiliana na Idara ya Magari, 120 State Street, Montpelier, VT 05603, kwa simu 802.828.2000, mtandaoni au katika ofisi ya DMV. Haya ni baadhi ya mambo unayopaswa kuzingatia kwa makini ikiwa umepata ajali.

1. Ni wapi hasa ilitokea.

2. Katika jiji, angalia majina ya barabara ikiwa ajali ilitokea kwenye makutano, au nambari ya nyumba iliyo karibu zaidi na ajali.
3. Nje ya miji, ni vigumu zaidi kuyatambua maeneo lakini ni muhimu pia.
4. Tafuta jina la mji ulio karibu, nambari ya njia au jina la barabara uliyoko, na jina na umbali wa kufikia makutano yaliyo karibu. Kumbuka ni umbali gani kutoka kwa kitu kama nguzo ya simu (kama ina namba), mwisho wa daraja, nyumba ya shambani, kivuko cha reli au namba iliyo karibu ya barabara kuu ya jimbo.
5. Alama za maili zinaweza kutumika kubainisha eneo kamili la tukio la ajali. Tumia habari hii kusaidia polisi wakati wa kuripoti ajali.
6. Wakati wa ajali.
7. Eleza ni uharibifu gani uliotokea.
8. Eleza ni majeraha gani yaliyopatikana katika ajali hiyo.
9. Pata jina, anwani, leseni na nambari za usajili za yule dereva mwingine. Pia ni vizuri kupata majina na anwani za abiria wa lile gari lingine na watu wote walioshudia ajali.

Kama umepata ajali na gari lingine, yule dereva mwingine ana haki ya kuona leseni yako, usajili na habari ya bima.

**Kumbuka: Kama dereva wa Vermont amepata ajali katika jimbo lingine, lazima iripotiwe katika jimbo ambalo ajali ilitokea.**

## LAZIMA UTUNZE VIZURI MAGARI YAKO

### Ukaguzi

Gari lako lazima likaguliwe mara moja kwa mwaka. Ukaguzi unahakikisha kuwa gari lako linakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka, lakini ni lazima ulitunze katika hali nzuri kila wakati. Ikiwa gari lako lina kasoro, unaweza kupatikana mwenye hatia kama kuna ajali.

Kibandiko cha ukaguzi huonyesha unapopaswa kupata ukaguzi unaofuata. Magari yote yanapaswa kukaguliwa ndani ya siku 15 za usajili, isipokuwa kama yana kibandiko halali cha ukaguzi wa Vermont.

## Vifaa vifuatavyo vinapaswa kuwa salama, kwa mpangilio mzuri wa kufanya kazi, na kurekebishwa ipasavyo:

### Breki

Baada ya muda breki huchakaa na lazima iwekwe bitana mpya. Mafuta au grisi yanaweza kuvuja kwenye breki na kuzifanya zinase. Maji yanaweza kuingia kwenye breki kutokana na kuendesha gari wakati wa mvua, na hivyo zisiweze kuzuia gari ipasavyo. Vumbi kutoka kwenye barabara za mchanga inaweza kuingia ndani na kuzichakaza. Kutumia breki mara nyingi kwenye safari ndefu katika nchi yenye vilima itafanya zipate joto kupita kiasi, na hazitafanya kazi vizuri. Breki lazima zikaguliwe mara kwa mara.

Sababu ya kawaida ya breki mbaya ni kwamba hazifanyi kazi pamoja vizuri. Wakati wa kutumia breki ghafla, moja inashika kabla ya nyingine na kusababisha gari yako kupinda. Unaweza kukagua hili mwenyewe kwa kuangalia kama gari linapinda upande mmoja unapoendesha kwa mwendo wa polepole kwenye barabara isiyo na magari mengine huku ukilishika usukani kwa wepesi.

Hakikisha kwamba kuna kioevu cha kutosha katika mfumo wa breki. Ukitambua kuwa kanyagio la breki linashuka chini sana, chunguza mafuta ya breki mara moja kwani kunaweza kuwa na uvujaji kwenye mfumo.

## Matairi

Matairi lazima yawe na angalau 2/32" ya kina cha kukanyaga. Si salama wala halali kutumia matairi ambayo kikanyagio kimeisha au yamebambuka kiasi kwamba yanaonyesha uchakavu kwenye tairi.

*Shikilia sarafu ya senti yenye mwili wa Abraham Lincoln kati ya kidole gumba na kidole cha shahada. Weka kichwa cha Lincoln kwanza kwenye mpasuko wenye kina kirefu zaidi. Je, unaweza kuona kichwa chake chote? Ikiwa ndiyo, matairi yako yamechakaa sana usiyaendeshee, na uhakikishe yamebadilishwa*

Hakikisha kuweka kiasi sahihi cha hewa kwenye matairi yako. Matairi yaliyojazwa kupita kiasi au yaliyo na hewa kidogo sana hupunguza mshiko wa barabara, husababisha matairi kuisha haraka, na kuathiri usukani. Kama gari lako linajivuta upande mmoja au usukani unakuwa mgumu, basi hakikisha magurudumu yako yamekaguliwa. Alama za mawimbi kwenye matairi ya mbele zinaweza kumaanisha kuwa magurudumu yako yamekosa ulingano. Jambo salama kufanya ni kuwa na matairi yote mazuri yenye kikanyagio cha kutosha.

## Usukani

Kama ni vigumu kuelekeza gari lako, au usukani unacheza sana, hakikisha umekaguliwa na makanika aliyehitimu. Kanuni nzuri ni kuhakikisha usukani wako unakaguliwa kile makanika huita "mwisho wa mbele" mara mbili kwa mwaka.

## Taa

Taa zako za mbele lazima ziwekwe katika hali nzuri ya kufanya kazi. Taa za mbele zinazofanya kazi ipasavyo na zinazotumika ifaavyo huonyesha kuwa dereva anafikiria usalama wa madereva wengine. Ikiwa taa zako za mbele zimefifia, zinalenga chini sana, au ni chafu, hutaweza kuona mbele kama unavyopaswa. Kama taa zinalenga juu sana au hazibadiliki kuwa mwali wa mwanga wa chini gari lingine linapokukaribia, taa zako zinaweza kumtia kiwi yule dereva mwingine.

Taa za nyuma, taa za kusimama, taa za kuashiria mwelekeo, na taa za maegesho zinapaswa kufanya kazi vizuri kila wakati. Nambari ya leseni ya nyuma lazima iwe na mwanga ili iweze kuonekana na kusomwa kwa angalau futi 50 kutoka nyuma ya gari. Balbu zinapoungua, zinapaswa kubadilishwa mara moja na zile zilizopendekezwa na mtengenezaji.

## Waipa za Kioo cha Mbele

Lazima uwe na waipa za kioo cha mbele zinazofanya kazi ipasavyo. Weka kioo cha mbele kikiwa safi, kwani hili huboresha uwezo wako wa kuona wakati wa kuendesha mchana na usiku.

## Madirisha na Viondoaukungu

Viondoaukungu vyote—mbele na nyuma—lazima viwe vikifanya kazi vizuri. Usijaribu kuendesha gari lolote kama sehemu za ndani za madirisha zina unyevunyevu na madirisha ya nje yamefunikwa na barafu au theluji. Hakikisha ndani ya madirisha yote ni safi.

## Mfumo wa Ekzosi

Mfumo wa ekzosi haupaswi kuvuja. Ekzosi inayovuja mara nyingi imesababisha sumu ya kaboni monoksidi au kifo kwa kuruhusu gesi ya monoksidi kaboni kuingia kwenye sehemu ya abiria ya gari. Huwezi kunusa gesi ya kaboni monoksidi. Ikiwa unasinzia au kuwa na kichefuchefu, inaweza kuashiria gesi ya kaboni monoksidi.

## Odometa na Spidometa

Spidometa na odometa kwenye gari lako lazima kifanye kazi vizuri na kiwe mahali ambapo dereva anaweza kukiona. Sheria ya serikali kuu inasema kuwa namba kwenye odometa hazipaswi kubadilishwa, na taarifa ya odometa lazima itiwe saini na muuzaji na mnunuzi wakati gari linauzwa.

## Mambo Mengine ya Kuzingatia

Dereva lazima aweze kuona vizuri mbele na kando ya gari, hivyo hakutakiwi kuwa na kitu chochote kinachozuia njia. Vitu vinavyobebewa ndani ya gari, abiria, au wanyama vipenzi havipaswi kumzuia dereva anapoendesha gari. Lazima uwe na kioo cha nyuma na honi. Sheria inasema hakutakiwi kuwa na kitu chochote kinachoning'inia kwenye kioo cha nyuma au viangazi vya jua.

## Mfumo wa Kudhibiti Utoaji wa Moshi

Magari ni chanzo kikuu cha uchafuzi wa hewa huko Vermont. Kwa pamoja, yanachangia zaidi ya 50% ya uchafuzi wa hewa unaozalishwa huko Vermont. Ingawa magari mapya ni safi zaidi (mradi yanatunzwa vizuri) kuliko miundo ya zamani, bado yanatoa kiasi kikubwa cha vichafuzi hewani. Ili kuhakikisha kwamba mfumo wa kudhibiti utoaji wa moshi wa gari lako unafanya kazi ipasavyo, hukaguliwa kama sehemu ya utaratibu wa ukaguzi wa kila mwaka.

Kama sehemu ya ukaguzi wa kila mwaka, kigeuza michemuo hukaguliwa ili kuhakikisha kwamba kipo kwenye gari lako. Ikiwa gari lako linatakiwa kuwa na kigeuza michemuo na hakipo au ikiwa kigeuza michemuo kimeharibika, lazima kibadilishwe. Ni kinyume cha sheria ya serikali kuu na ya jimbo kutenganisha kigeuza michemuo cha gari lako au kumruhusu makanika kukiondoa au kukiharibu.

Njia nyingine ambayo magari husababisha uchafuzi wa hewa ni kupitia mvukizo wa gesi. Wakati wa ukaguzi wa kila mwaka, kifuniko cha tanki la mafuta la gari lako kitakaguliwa ili kuhakikisha kuwa kiko katika hali nzuri.

Mfumo wa kompyuta wa Uchunguzi wa Bodi (OBD) utakaguliwa ili kuhakikisha mfumo wa kudhibiti utoaji wa moshi ya gari unafanya kazi vizuri. Maeneo maalum ya tatizo yanaweza kugunduliwa kupitia "OBD" inayofanya kazi ipasavyo.

Ili kujua zaidi kuhusu utoaji wa moshi ya magari na unachoweza kufanya ili kusaidia kuweka hewa ya Vermont iwe safi iwezekanavyo, tembelea tovuti ya Mamlaka ya Maliasili pale mtandaoni.

**Maswali kuhusu mpango wa ukaguzi wa kila mwaka yanaweza kuelekezwa kwa Idara ya Magari kwa simu (802) 828-2094.**

## Mikanda ya Usalama

Sheria inahitaji abiria wote wa gari wazuiliwe kwa mkanda wa usalama, au mfumo wa kuzuia abiria mtoto ulioidhinishwa na serikali kuu.

### Kuvaa Mkanda Wako wa Usalama

Unapovaa mkanda wa usalama (au mkanda wa kiti), kuna uwezekano mdogo wa wewe kujeruhiwa au kuuawa katika ajali. Mikanda ya usalama hufanya iwe rahisi kukaa katika nafasi salama na ya kustarehesha kwa udhibiti bora wa gari; mikanda ya usalama hukushikilia katika nafasi ambayo watengenezaji wa magari walikusudia uwe.

Mikanda ya usalama ni bora zaidi inapotumiwa ipasavyo. Mikanda ya kiunoni inapaswa kuwekwa vizuri kwenye nyonga, sio juu ya tumbo. Mikanda ya bega huenda juu ya bega na kupitia katikati ya kifua. Upanuzi ya mikanda ya usalama inapatikana kutoka kwa mtengenezaji wa gari. Kamwe usiweke ukanda wa bega chini ya mkono wako au nyuma ya mgongo wako. Mikanda ya usalama imeundwa kupita mwilini kwenye sehemu zake zenye nguvu zaidi ili kukulinda wakati wa ajali ya gari. Mikanda ya usalama hukuweka ndani ya gari, katika nafasi moja, badala ya kutupwa nje ya gari ambapo uwezekano wa kifo na majeraha mabaya ni mkubwa zaidi. Matumizi ya mikanda ya usalama huweka abiria katika nafasi moja ndani ya gari ambapo pia nafasi za kujeruhiwa na abiria wengine hupunguzwa wakati wa ajali.

### Mlinde Mtoto Wako - ni Sheria!

Ajali za magari ndiyo sababu kuu ya vifo vya watoto wenye umri wa miaka 3 hadi 14. Wazazi na walezi wanahimizwa kuhakikisha kwamba viti vya watoto na viti vya kuongeza urefu vimefungwa vizuri kwenye magari yao ili kuzuia majeraha na vifo vya watoto wao.




Katika visa vingi, wazazi wanachanganyikiwa kuhusu jinsi ya kufunga kiti cha mtoto wao kwa usahihi, hawajui kwamba kila kiti hakiwezi kutoshea kwenye kila gari, au hawatambui kwamba gari lao limewekewa mfumo wa Nanga za Chini na Kamba za Watoto (LATCH). Karibu kila kiti cha gari na magari mengi yaliyotengenezwa tangu Septemba 1, 2002, yanahitajika kuwa na mfumo wa LATCH. LATCH hufanya iwe rahisi kufunga kiti cha mtoto kwa usahihi – mara ya kwanza na kila mara.

Kwa habari zaidi kuhusu kuchagua kiti sahihi au kupata mahali pa Bila malipo pa Ukaguzi wa Usalama wa Viti vya Watoto palipo karibu nawe, tembelea Be Seat Smart.

### Watoto wachanga - kuanzia kuzaliwa hadi angalau umri wa mwaka mmoja na angalau ratili 20

Kwa ulinzi bora zaidi, waweke watoto wachanga kwenye kiti cha nyuma, kwenye viti vya usalama vya watoto vinavyoangalia nyuma, kwa muda mrefu iwezekanavyo hadi kufikia kiwango cha juu cha urefu au uzito wa kiti husika. Kwa kiwango cha chini, sheria ya jimbo inahitaji kuweka watoto wachanga wakiwa wakiangalia nyuma hadi wafikie umri wa mwaka mmoja na angalau ratili 20.

### Watoto wadogo - umri wa mwaka mmoja na ratili 20 hadi umri wa miaka minne na ratili 40

Watoto wanapokuwa wakubwa na kutoka kwenye viti vyao vya kuangalia nyuma, wanatakiwa kukaa kwenye viti vya usalama vya watoto vinavyoangalia mbele, kwenye kiti cha nyuma, hadi wafikie kiwango cha juu cha uzito au urefu wa kiti husika.

**Watoto - kuanzia umri wa miaka minne hadi angalau umri wa miaka minane**

Watoto wanapokuwa wakubwa na kutoka kwenye viti vyao vinavyokabili mbele, wanatakiwa kukaa kwenye viti vya kuongeza urefu, kwenye kiti cha nyuma, hadi mikanda ya gari iweze kutoshea vizuri. Mikanda ya usalama inatoshea vizuri pale mshipi wa kiunoni unapokaa vizuri kwenye nyonga na kugusa mifupa ya nyonga, na mshipi wa bega unakaa vizuri kifuani ukigusa mfupa wa kidari.

**Vijana - umri wa miaka minane na zaidi.**

Unapomhamishia mtoto kutoka Kiti cha Kuongeza Urefu hadi kiti cha gari, miguu ya mtoto inapaswa kufika sakafuni huku magoti yakiwa yamepinda na mgongo wake ukiwa umeshikamana na mgongo wa kiti. Watoto wanaweza kutumia mkanda wa usalama wa watu wazima kwenye kiti cha nyuma ikiwa unawatoshea vizuri (mkanda wa kiunoni unakaa vizuri kwenye nyonga na kugusa mifupa ya nyonga, na mkanda wa begani unakaa vizuri kifuani na kugusa mfupa wa kidari).

**KUMBUKA: Kamwe usiweke kiti cha usalama cha mtoto mbele ya mfuko wa hewa!**



# Sura ya 8 - Mfumo wa Pointi

## Mfumo wa Pointi wa Vermont

Pointi huwekwa kwenye rekodi yako ya kuendesha gari kila wakati unapopatikana na hatia ya kuvunja sheria ya magari. Kwa mfano, unapewa pointi kwa makosa yafuatayo:

1. Kasi, pointi 2 - 8 kulingana na kasi yako juu ya kikomo cha kasi.
2. Kutuma ujumbe unapoendesha gari, pointi 2 - 5.
3. Kuendesha gari bila leseni, pointi 2.
4. Kukosa kusimama kwa ishara ya kusimama au taa nyekundu, pointi 2.
5. Kukosa kumtii afisa wa polisi, pointi 4.
6. Kukosa kutoa haki ya njia kwa gari la wagonjwa, gari la moto, afisa wa polisi, pointi 5.
7. Kukosa kutoa haki ya njia kwa mtembea kwa miguu katika kivuko, pointi 4.
8. Kukosa kusimama kwa ajili ya basi la shule lililosimama lenye taa nyekundu za onyo zinazowaka, alama 5.

Dereva anapopokea jumla ya pointi 10, anatumiwa barua kumjulisha kwamba haki yake ya kuendesha gari itasimamishwa. Kikao chaweza kuombwa kuthibitisha hukumu na idadi ya pointi zilizokusanywa. Idadi ya pointi zilizopokewa ndani ya miaka 2 itaamua muda gani haki yako ya kuendesha gari itasimamishwa. Pointi nyingi zinavyopokelewa - ndivyo muda utakavyokuwa mrefu wa kusimamishwa. Pointi hazitathminiwi kwa ajili ya maegesho au ukiukaji wa vifaa vyenye kasoro.

# Sura ya 9 - Umiliki wa Gari

## JINSI YA KUSAJILI GARI LAKO

Hii ni habari ya msingi juu ya usajili wa gari. Kwa maelezo ya kina tafadhali piga simu 802.828.2000 au ututembelee mtandaoni kwa dmv.vermont.gov. Kama unaishi Vermont na una gari ambalo unataka kuendesha barabarani, lazima ulisajili. Kama unahamia Vermont kutoka jimbo lingine, lazima usajili gari lako ndani ya siku 60 za kuhamia jimboni.

### Usajili na Mabamba

Thibitisho la usajili halali lazima liwe kwenye gari kila wakati linapotumiwa. Afisa wa polisi ana haki ya kuliona. Mabamba ya usajili lazima yabandikwe vizuri ili yasilegee. Hakuna sehemu ya bamba ya usajili inapaswa kufunikwa au kufichwa ili isionekane, na ni lazima ziwe safi nyakati zote. Bamba la nyuma ni lazima limulikwe ili liweze kusomeka kutoka umbali wa angalau futi 50 . Mabamba ya nambari unayopewa lazima yatumike tu kwa gari hilo. Unaweza kuyahamishia kwa gari lipya unalolinunua kama unabadilishana au ukiuza gari lako la zamani.

### Kuuza gari lako kwa mtu mwingine:

1. Mpe mmiliki mpya hati ya mauzo inayojumuisha jina la mnunuzi, sahihi ya muuzaji, tarehe ya mauzo, mwaka, muundo, nambari asilia na kiasi cha pesa ulicholipwa kwa gari.
2. Saini sehemu ya nyuma ya cheti cha umiliki ikionyesha jina na anwani ya mmiliki mpya. Pia jaza idadi ya maili ya gari na tarehe ya mauzo.
3. Taarifa ya odometa inahitajika kusainiwa na muuzaji na mnunuzi kwa mauzo yote ya magari ya mwaka wa 2011 au mapya zaidi. Taarifa hii imejumuishwa kwenye cheti cha umiliki wa gari lako na/au Hati ya Mauzo ya Vermont.
4. Ondoa mabamba yako ya usajili kutoka kwa gari.

### Kubadilishana gari lako:

1. Mpe mmiliki mpya hati ya mauzo inayojumuisha jina la mnunuzi, sahihi ya muuzaji, tarehe ya mauzo, mwaka, muundo, namba ya asilia, na kiasi ulicholipwa au ulilchojuzika kwa kubadilishana gari lako la zamani.
2. Muombe mtu unayebadilishana naye akupe hati ya mauzo ya gari unalopata. Hii inapaswa kuwa na maelezo kuhusu gari ulilobadilishana nalo. Hakikisha cheti cha umiliki wa gari kimesainiwa ifaavyo kwako.
3. Ondoa bamba lako za usajili kutoka kwa gari la zamani. Kama unataka kuhamisha usajili wako, liweke bamba kwenye gari ulilonunua sasa hivi.
4. Jaza Fomu ya Maombi ya Usajili, Kodi na Cheti cha Umiliki, na ujumuishe cheti cha umiliki wa gari ulilonunua. Tuma fomu hizi pamoja na hundi au hawala ya fedha ya ada sahihi kwa Idara ya Magari huko Montpelier ndani ya saa 24.

### Usajili uliopotea au Mabamba ya Usajili

Ukipoteza cheti chako cha usajili, unaweza kupewa kingine kule Idara ya Magari katika ofisi yoyote yetu, kwa barua, au mtandaoni kupitia dmv.vermont.gov.

Ukipoteza bamba moja la usajili au yote mawili, chukua Fomu ya Maombi ya Kupewa Bamba ingine katika ofisi yoyote ya Idara ya Magari, kituo cha polisi, au mtandaoni kupitia dmv.vermont.gov.

### Jina/Anwani/Mabadiliko ya Gari

Ukibadilisha jina lako, anwani yako au rangi ya gari lako, unahitajika kuijulisha Idara ya Magari ndani ya siku 30.

## Kodi ya Ununuzi na Matumizi

### Magari Yasiyokodishwa

Unaponunua gari jipya au lililotumika, ni lazima ulipie ushuru. Hii inaitwa Kodi ya Ununuzi na Matumizi na ni 6% ya bei uliyolipia gari lisilokodishwa au thamani ya sasa ya soko, chochote kilicho kikubwa zaidi.

Wakazi wapya wa Vermont wanaoomba usajili kwa mara ya kwanza kwa gari lililonunuliwa nje ya Jimbo la Vermont ambalo kodi ya mauzo au matumizi imelipwa na mtu anayeomba usajili Vermont, au mwenzi wake, watasamehewa Kodi ya Ununuzi na Matumizi ya Vermont baada ya kutoa ushahidi kwamba kodi iliyolipwa katika eneo lingine ni sawa na au zaidi ya kodi ya Vermont au kama gari limesajiliwa katika eneo linalokusanya kodi ya Ununuzi au Matumizi kwa angalau miaka 3. Kama kodi iliyolipwa katika eneo lingine ni ndogo kuliko kodi ya Vermont, kodi inayopaswa kulipwa itakuwa kiasi kinachobaki.

### Magari ya Kukodisha

Maombi yote ya usajili, kodi, na/au cheti cha umiliki wa gari lililokodishwa kutoka kwa muuzaji wa magari wa Vermont au muuzaji wa magari wa Vermont anayefanya kazi kwa niaba ya mkodishaji, lazima yaambatane na Fomu ya Mkokotoo wa Kodi ya Ununuzi na Matumizi - Fomu ya Gari Lililokodishwa (VD-147) au nakala ya mkataba wa kukodisha na/au karatasi ya kazi ya muuzaji. Ikiwa stakabadhi zinazofaa hazitapokelewa, gari lililokodishwa litatozwa kodi ya 6% ya gharama ya ununuzi.

Gharama inayotozwa kodi ya gari lililokodishwa itahesabiwa kwa 6% ya gharama ya ununuzi wa gari, ukiondoa thamani ya mwisho wa mkataba, kama ilivyoainishwa kwenye Fomu ya Mkokotoo wa Kodi ya Ununuzi na Matumizi - Gari Lililokodishwa (VD-147) au kama ilivyoainishwa kwenye mkataba wa kukodisha na/au karatasi ya kazi ya muuzaji, bila kujali ikiwa una chaguo la kununua gari mwishoni mwa mkataba wa kukodisha au la.

## Maelezo ya Cheti cha Gari

Magari yote lazima yawe na Cheti cha Magari cha Vermont. Baadhi ya vitu vya pekee ni: pikipiki yenye ujazo wa injini chini ya 300 cc na trela yenye uzito tupu wa ratili 1,500 au chini ya hapo.

Cheti cha Asili cha Mtengenezaji kinahitajika kwa magari yote mapya. Huwezi kusajili gari bila ya hii.

Magari yote yanayosajiliwa katika Vermont lazima yawe na ombi la usajili. Pia utahitaji hati ya mauzo na cheti cha mmiliki wa awali kilichosainiwa ili kuhamishwa kwa jina lako.

**Nambari ya Utambulisho wa Gari (VIN)**

Nambari ya Utambulisho wa Gari (VIN) ni msimbo wa kutambua **Gari** maalum. VIN ina herufi 17 (nambari na herufi kubwa) ambazo hutumika kama kitambulisho cha kipekee kwa gari. VIN huonyesha sifa za kipekee za gari, uhalisi, na mtengenezaji. Kabla ya 1981, VIN zilitofautiana kwa urefu kutoka herufi 11 hadi 17.

Wakati Uthibitisho Unahitajika

- Magari yenye Nyaraka za Kuokoa.
- Magari yanayotolewa hati ya umiliki kwa dhamana.
- Magari yenye usajili kutoka nchi yoyote ya kigeni, ikiwa ni pamoja na Kanada.

Uthibitishaji wa VIN lazima ukamilishiwe Vermont. Uthibitishaji wa VIN unapaswa kukamilishwa na afisa wa kutekeleza sheria wa Vermont, wafanyakazi walioajiriwa na kitengo cha utekelezaji wa sheria ambao, kwa kusudi hili, wako chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa afisa wa utekelezaji wa sheria, au wafanyakazi wa DMV walioteuliwa na Kamishna wa Magari wa Vermont.

**Magari Yaliyokarabatiwa:**

Magari Yote Yaliyosajiliwa Vermont ambayo yana cheti cha **KUOKOLEWA** yatapewa cheti cha umiliki chenye maneno **GARI YAKUKARABATIWA**. Unapoomba kusajili gari la **KUOKOLEWA** lazima uwe na namba ya utambulisho wa gari (VIN) iliyokaguliwa na mfanyakazi wa Idara ya Magari au afisa wa utekelezaji wa sheria wa Vermont na kukamilisha sehemu ya uthibitisho wa VIN kwenye ombi.

**Rehani**

Ukikopa pesa kununua gari kutoka benki, shirika la mikopo, au mtu mwingine, gari hilo linasemekana kuwa na "reheni" kwalo. Mtu au benki unayekopa kutoka kwake huitwa "mhifadhi wa rehani." Jina la mhifadhi wa rehani lazima liwekwe kwenye ombi la usajili. Cheti cha umiliki wa gari lako, kitakapotolewa, kitatumwa kwa mhifadhi wa rehani na hutapewa mpaka ulipie pesa ulizokopa.

**Bima**

Vermont ina sheria inayoitwa "Utunzaji wa Uwajibikaji wa Kifedha." Hii inamaanisha kuwa gari unaloendesha LAZIMA liwe na bima ya dhima.

Dhima na uharibifu wa mali ni aina muhimu zaidi ya bima ya gari unayopaswa kuwa nayo. Hukukinga dhidi ya hasara ya kifedha wakati majeraha ya mwili au uharibifu wa mali unapotekea.

Kiwango cha bima KINAPASWA kuwa angalau $25,000 kwa kifo au majeraha ya mtu mmoja; $50,000 kwa kifo au majeraha ya watu 2 au zaidi; $10,000 kwa uharibifu wa mali. Lazima ubebe kadi kutoka kwa kampuni yako ya bima ndani ya gari inayoonyesha kuwa kuna bima ya gari hilo. Unaposimamishwa na afisa wa polisi, utalazimika kuonyesha kadi hiyo. Kama unaenda kufanya mtihani wa udereva pia utalazimika kuonyesha kadi hiyo.

Ikiwa afisa wa polisi atakusimamisha na kukuomba uonyeshe uthibitisho wa bima yako na huna bima, afisa huyo atakupa tiketi. Utapigwa faini na kutozwa pointi mbili kwenye rekodi yako ya udereva.

Ikiwa una bima kwenye gari lako na afisa wa polisi akusimamishe, na huwezi kuonyesha kadi hiyo kwa afisa, una siku 15 za kufanya hivyo. Kadi unayoonyesha afisa lazima iseme kuwa ulikuwa na bima afisa huyo alipokusimamisha.

Kama unaendesha gari bila bima na mojawapo ya yafuatayo yatatokee, leseni yako itachukuliwa na Kamishna wa Magari hadi upate bima. Lazima uthibitishe kwa Kamishna kuwa una bima kwa miaka 3 kamili.

- Uko katika ajali, hata kama sio kosa lako,
- Kuendesha gari ukiwa na umekunywa pombe au madawa ya kulevya,
- Kuendesha gari au kuchukua gari la mtu mwingine bila idhini ya mmiliki,
- Kuendesha gari wakati leseni yako imesimamishwa, kufutwa, au kukataliwa,
- Kuendesha gari kwa njia ya kusababisha kifo cha mtu mwingine,
- Kuondoka eneo la ajali

**Ukaguzi (tazama ukurasa wa 62 kwa maelezo zaidi)**

Gari lako lazima likaguliwe mara moja kwa mwaka. Ukaguzi unahakikisha kuwa gari lako linakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka, lakini ni lazima ulitunze katika hali nzuri kila wakati. Ikiwa gari lako lina kasoro, unaweza kupatikana mwenye hatia kama kuna ajali.

Kibandiko cha ukaguzi huonyesha unapopaswa kupata ukaguzi unaofuata. Magari yote yanapaswa kukaguliwa ndani ya siku 15 za usajili, isipokuwa kama yana kibandiko halali cha ukaguzi wa Vermont.

**Endesha Nadhifu na Uweke akiba - Vidokezo vya "Green Driving".**

Hapa kuna vidokezo 10 bora vya kuendesha gari ambavyo vitakuokolea pesa ya petroli, kupunguza kiwango chako cha kaboni, na kuhifadhi nishati!

**PUNGUZA MWENDO NA KUANGALIA KASI**- Kwenye barabara kuu ya jimbo, endesha maili 55 au 60 kwa saa badala ya 65 ili kuokoa mafuta. EPA inakadiria kuboreshwa kwa hadi asilimia 15 katika uchumi wa mafuta kwa kufuata kidokezo hiki pekee.

**ONGEZA MWENDO NA KUKANYAGA BREKI KWA WEPESI** - Kuongeza mwendo kwa utaratibu kutoka kusimama na kukanyaga breki kwa upole huhifadhi mafuta. Kuanza kwa kasi, kupindapinda ndani na nje ya trafiki na kukanyaga breki kwa nguvu huharibu mafuta na kuchakaza baadhi ya vifaa vya gari, kama vile breki na matairi, haraka zaidi. Ongeza kasi ya gari lako kwa kudumisha umbali salama kati ya magari na kutarajia hali ya trafiki ili kuruhusu muda zaidi wa kukanyaga breki na uongeze mwendo hatua kwa hatua.

**EPUKA KUGURUMISHA GARI KWA MUDA MREFU UKIWA UMEEGESHA** - kugurumisha gari huharibu mafuta, husababisha kuzeeka kwa injini, na kunaweza kusababisha magonjwa ya kupumua. Katika majira ya baridi, ondoa theluji na barafu kutoka kwa madirisha kabla ya kugurumisha injini. Usalama kwanza: ikiwa kuondoa ukungu hakutoshi, ongeza muda wa kupasha joto ikihitajika. Punguza kupasha joto wakati gari limesimama hadi sekunde 30 inapowezekana. Kuendesha gari polepole hadi wastani ni njia bora zaidi ya kupasha joto. Ikiwa umeegesha mjini, kugurumisha kwa zaidi ya sekunde 10 hutumia mafuta zaidi kuliko kuzima na kuwasha upya. Kuruhusu gari ligurume bila uangalizi hadharani ni ukiukaji wa sheria ya magari yasiyotunzwa ya Vermont; ukiacha gari lako, lazima ulizime.

**KAGUA TAIRI ZAKO** - Hakikisha matairi yamejazwa hewa ipasavyo kwa shinikizo linalopendekezwa (ambalo unaweza kulipata kwenye kibango kilichoko kwenye mlango wa upande wa dereva uliobanwa na pia kwenye mwongozo wa mmiliki wa gari). Hili peke yake inaweza kupunguza kiwango cha wastani cha matumizi ya mafuta kwa asilimia 3-4

. Matairi yaliyo na hewa duni huongeza kinzi ya kubingirika na kupunguza uchumi wa mafuta. Huwa yanaisha haraka zaidi pia.

**KUWA MKARIMU KWA GARI LAKO** - Dumisha ulinganifu sahihi wa injini ili kuweka magari yakifanya kazi kwa ufanisi. Weka magurudumu yakilinganika. Magurudumu yanayopigana yenyewe kwa yenyewe huharibu mafuta. Badilisha vichujio vya hewa kama inavyopendekezwa. Daima tafuta ushauri kwenye Mwongozo wa Mmiliki kwa matengenezo sahihi.

**SAFIRI NA MIZIGO MICHACHE** - Uzito usiohitajika, kama vile vitu visivyo lazima kwenye buti na mizigo mingi kwenye keria ya paa, hufanya injini kufanya kazi ya ziada na hutumia mafuta zaidi.

**PUNGUZA MATUMIZI YA JOTO NA KIYOYOZI** - Tumia joto na kiyoyozi kwa uangalifu ili kupunguza mzigo kwenye injini. Kupunguza matumizi ya kiyoyozi wakati halijoto linapita nyuzi 80 kunaweza kusaidia kuhifadhi mafuta ya asilimia 10-15. Tumia mipangilio ya hewa kadri iwezekanavyo. Egesha gari kwenye kivuli ili kuweka gari baridi kidogo na kupunguza haja ya kiyoyozi.

**FUNGA MADIRISHA KATIKA MWENDO WA KASI** - Usiendeshe gari madirisha yakiwa wazi isipokuwa kasi yako iwe chini ya maili 50 kwa saa. Kuendesha gari madirisha yakiwa wazi kwa mwendo wa barabara kuu huongeza mvuto wa hewa kwenye gari na kupunguza ufanisi wa matumizi ya mafuta.

**UNGANISHA SAFARI** - Panga KImbele ili kuunganisha safari zako, kuokoa maili nyingi za kusafiri. Kupanga kimbele pia kutakuwezesha kupita njia zenye msongamano, na kupunguza gari kuguruma kama imesimama.

**UBIA WA GARI** - Tumia gari lako na wengine ukienda kazini, katika ununuzi na burudani. Haiokoi petroli tu, inaweza kuwa raha zaidi kuliko kuendesha gari peke yako.

# Sura ya 10 - Leseni ya Kibiashara

**<u>LESENI YA DEREVA YA KIBIASHARA</u>**

Leseni ya Dereva wa Biashara inahitajika kwa waendeshaji wa magari yaliyopitisha kiasi cha ratili 26,000 au kusafirisha abiria 16 au zaidi (ikiwa ni pamoja na dereva) au vifaa hatari. Kuna madaraja tatu ya Leseni ya Dereva wa Kibiashara:

- **Daraja A** - Mchanganyiko wowote wa magari yenye GCWR ya ratili 26,001 au zaidi, mradi kitengo kinachokokotwa kina GVWR ya ratili 10,001 au zaidi.
- **Daraja B** - Gari moja moja ya GVWR ya ratili 26,001 au zaidi, mradi gari lolote linalokokotwa lina GVWR ya ratili 10,000 au chini.
- **Daraja C** - Gari moja moja ya GVWR ya ratili 26,000 au chini, yanayosafirisha bidhaa hatari zenye mabango au yaliyoundwa kubeba abiria 16 au zaidi ikiwa ni pamoja na dereva. Magari haya yanaweza kukokota gari la GVWR la ratili 10,000 au chini.
- **Kibali cha Maelekezo ya Udereva ya Kibiashara (Mwanafunzi)** - inaruhusu mtu kupokea mafunzo ya kuendesha gari ya kibiashara na uzoefu wa usukani kwenye barabara kuu za umma.

Kwa mujibu wa sheria ya jimbo na serikali kuu, mtu yeyote anayeshikilia Leseni ya Kibiashara kutoka jimbo lingine lazima ahamishe Leseni ya Dereva ya Kibiashara ndani ya siku 30 za kuanza kuishi huko Vermont.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Leseni za Dereva ya Kibiashara na vibali vya kufundisha piga simu 802.828.2000.

Kupanga ziara ya mtihani wa kuandika tembelea mydmv.vermont.gov. Ili kupanga jaribio la ustadi wa CDL, lazima kwanza uwasilishe ada ya ratiba kwa: CDL Unit, Department of Motor Vehicles, 120 State St., Montpelier, VT 05603-0001. Mara ada inapopokelewa, unaweza kupanga jaribio la ustadi.

Mwongozo wa Leseni ya Dereva ya Kibiashara ya Vermont unapatikana katika Ofisi zote za Idara ya Magari.



## Sura ya 11 - Watu wenye Ulemavu

Idara ya Magari inajua jinsi ilivyo muhimu kwako kuendesha gari. Mtu ambaye ana ulemavu bado anaweza kupata leseni. Gari linaweza kuhitaji vifaa maalum ili kuliendesha kwa usalama. Ikiwa mtu mwenye ulemavu anahitaji kifaa maalum, ni lazima kitoshee na kifanye kazi ipasavyo.

Unapofanya jaribio lako, kuwa mkweli katika kuelezea ulemavu wako kwa mtahini. Kama unahitaji msaada kuingia kwenye jengo ambalo utafanyia jaribio, mjulishe mpangaji unapopiga simu kufanya miadi yako.

Kama una shida ya matibabu kama vile kifafa, ugonjwa wa kisukari (kuhitaji sindano ya insulini), au hali nyingine yoyote ambayo inaweza kusababisha kupoteza fahamu au kupoteza kiungo au uko kwenye kiti cha magurudumu, lazima ujulishe Idara ya Magari, Kitengo cha Uboreshaji wa Dereva kwa 802.828.2000 kabla ya kufanya miadi ya mtihani. Utatumiwa fomu ya tathmini ya matibabu ambayo lazima ikamilishwe na daktari wako. Daktari atakapokamilisha fomu, itume kwa Idara ya Magari kwa ajili ya ukaguzi. Utaarifiwa kwa maandishi ikiwa idhini imetolewa au haijatolewa ili upewe Kibali cha Mwanafunzi. Ikiwa huna uhakika kama hali ya kiafya uliyo nayo itaathiri uwezo wako wa kupata Kibali cha Mwanafunzi, tafadhali piga simu kwa Idara ya Magari, Kitengo cha Uboreshaji wa Madereva kwa nambari 802.828.2000 kwa ushauri.

**Maegesho ya Madereva Walemavu**

Mtu ambaye ana shida ya kutembea anaweza kuegesha bila ada, kwa siku 10, katika eneo la maegesho ambapo madereva wengine wanaweza tu kuegesha wakati uliowekwa. (Watu kama hao hawawezi kuegesha katika mahali ambapo maegesho au kusimamisha magari hairuhusiwi. Hawawezi kuegesha katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa magari fulani, au mahali popote ambapo maegesho yamepigwa marufuku.) Ili kufanya hivyo, mtu lazima awe na bamba maalum ya usajili au bango ambalo limetolewa na Idara ya Magari ya Vermont, au bamba maalum ya usajili au kifaa kingine ambacho kimetolewa na jimbo lingine kwa madhumuni ya maegesho ya walemavu. Mtu mlemavu anaweza kupata seti ya Mabamba ya Usajili wa Walemavu kwa kila gari lililosajiliwa kwa jina lake. Hakuna ada ya ziada kwa mabamba haya kama gari tayari limesajiliwa Vermont. Ikiwa mtu mlemavu hana gari au hataki Mabamba ya Usajili wa Walemavu, mtu huyo anaweza kupata Bango la Maegesho la Walemavu. Bango la Maegesho la Walemavu pia linapatikana kwa abiria vipofu.

Mtu, ambaye ni mlemavu au shirika linalotoa Nambari yake ya Kitambulisho cha Shirikisho, anaweza kuomba kadi ya Maegesho ya Walemavu. Hakuna ada ya bango. Fomu inaweza kupatikana kutoka Idara ya Magari, Ofisi za Polisi za Jimbo, au ofisi za Karani wa Jimbo. Utahitaji kujaza fomu fulani na daktari wako atalazimika kujaza sehemu nyingine ya fomu.

Mabamba ya Walemavu/Bango la mlemavu laweza kufutwa ikiwa mlemavu huyo anaruhusu watu wasio walemavu kutumia vibaya fadhila za Mabamba yao ya Maegesho/Bango la Walemavu.

Mtu anayeegesha katika maegesho ya walemavu kinyume cha sheria anaweza kutozwa faini na gharama za kuliondoa.

Kwa mujibu wa 9 V.S.A. §4110, mwendeshaji wa gari ambaye amepewa Bamba la Walemavu au Bamba la Maegesho chini ya sheria za Jimbo la Vermont au jimbo lingine lolote atapata huduma kamili na kila kituo cha petroli kinachoonyesha Ishara ya kimataifa

wa ufikiaji wa ulemavu na, katika vituo vya petroli vya huduma kamili vinavyotoa huduma ya kujitegemea kwa gharama ndogo, atapokea kiwango kidogo.

Vituo vya petroli vya huduma ya kibinafsi, wakati wa ombi na mwendeshaji wa gari ambaye anamiliki Bamba la Walemavu au Bamba la Kuegesha, atahitaji mhudumu kutoa petroli kwa gharama ya huduma ya kibinafsi.

**Kodi ya Ununuzi na Matumizi kwa Madereva Walemavu**

Gari moja linalomilikiwa au kukodishwa na mlemavu au mzazi au mlezi wake ambalo lina vifaa maalum wakati wakusajiliwa na mtu huyo halitatozwa kodi ya ununuzi na matumizi. Ikiwa unakidhi vigezo vifuatavyo, unaweza kuwa na haki ya kuondolewa kutolipa ushuru wa ununuzi na matumizi:

1. Lazima uwe na ulemavu ambao umekufanya uwe mlemavu kabisa.
2. Vidhibiti vya gari lazima vibadilishwe ili kukuwezesha kuendesha gari, au lazima iwe na kifaa cha kuinua mitambo ili kuwezesha gari kuingia na kutoka.
3. Leseni yako ya Dereva lazima izuiliwe ili kufanya kazi na vidhibiti vilivyobadilishwa, kama unadai ondoleo kwa sababu ya usakinishaji wa vidhibiti vilivyobadilishwa.
4. Wewe na wamiliki wengine wa cheti/wasajiliwa mnaweza kuwa na usajili mmoja tu unaohusisha ondoleo la kodi ya ununuzi na matumizi kwa wakati mmoja.
5. Fomu VT-014 iliyosainiwa na daktari.

## Sura ya 12 - Wazazi au Walezi

Ajali za magari ndizo sababu kuu ya vifo na majeraha kwa vijana. Kama mzazi au mlezi, una jukumu muhimu la kushawishi tabia salama za mtoto wako za kuendesha gari.

1. Hakikisha kijana wako ana nafasi nyingi za kufanya mazoezi ya kuendesha gari, hata zaidi ya saa 40 zinazohitajika.

2. Weka mfano mzuri kama dereva salama, anayewajibika, na anayefuata sheria.

3. Weka na kujadili sheria za familia za kudumisha haki za kuendesha gari kulingana na sababu zinazojulikana za hatari kwa madereva vijana. Kanuni kama hizo zinaweza kushughulikia:

   - Ukosefu wa matumizi ya mkanda wa usalama
   - Mwendo wa kasi
   - Kuendesha gari usiku (baada ya saa 9 usiku)
   - Kutumia simu ya mkononi au mivuto mingine ya mawazo
   - Abiria wengi vijana
   - Kuendesha gari ukiwa na usingizi
   - KUENDESHA GARI KAMA UMEDHURIKA

4. Msaidie kijana wako kuelewa hatari zinazohusiana na kuendesha gari na dereva mwingine wa kijana, hasa wale ambao huchagua kuendesha gari kwa hatari na/au kukiuka sheria.

5. Wasiliana na mtoto wako na wazazi wengine ili kuwasaidia wote, madereva na abiria, kufuata masharti ya Leseni ya Dereva Kijana. Hii itasaidia vijana wote kukaa salama na ndani ya sheria ya GDL.

6. Mhimize kijana wako kuzungumzia usalama anapoendesha gari na madereva wengine.

7. Chagua gari salama, la kuaminika, lililohifadhiwa vizuri kwa dereva wako kijana.

(Tembelea www.iihs.org/ratings kwa ukadiriaji wa ajali ya magari na habari zingine kuhusu kuchagua magari salama kwa vijana)

KUMBUKA: Kibali cha Mwanafunzi na Leseni ya Dereva Kijana ni "za muda" na zinaweza kusitishwa.

- Kama mzazi au mlezi, unaweza kusimamisha leseni ya muda ya mtoto wako kwa kuandika kwa Kamishna wa Idara ya Magari
- Mapendekezo kutoka kwa Bodi ya Mchepuo/Urekebishaji yanaweza kusababisha kusitishwa siku 30

**Imedondolewa kutoka kwa - MWONGOZO WA MZAZI KWA LESENI YA DEREVA YA HATUA KWA HATUA (GDL)**

Pombe, 7, 52, 53

Wanyama, 19

Kuzuia Kukwama, 48, 49

Baiskeli, 40, 52

Simu ya mkononi, 47, 56, 73

Kiti cha Mtoto, 62

Leseni ya Dereva ya Kibiashara, 12, 17, 70

Anwani ya sasa, 8, 10

Tarehe ya Kuzaliwa, 8

Waliovutwa Mawazo, 54, 55

Elimu ya Udereva, 12, 13, 14, 15

Kadi ya Haki ya Dereva, 11, 12

Dawa, 52, 53, 58, 68

Gari la Dharura, 31,

Mfumo wa Udhibiti wa Uzalishaji wa Gesi

Sumu 51, Leseni ya Dereva ya 61, 9, 12

Raia wa kigeni, 9

Sekunde Nne, 27, 28, 46

Jinsia, 11

Ishara ya Mkono, 26, 41

Taa za Mbele, 19, 25, 42, 45, 46, 49, 51, 60

Alama za Barabara Kuu, 34

Utambulisho, 4, 8, 9

Idhini Iliodokezwa, 53

Barabara kuu za jimbo 28, 31, 38, 40, 50, 51, 59

Leseni ya Dereva Kijana, 7, 12, 13, 14,

15, 20, 21, 23, 73

Kibali cha Mwanafunzi, 2, 3, 7, 12, 13, 15,

16, 20, 21, 23, 24, 25, 71, 73

Mageuko ya Kushoto , 26

Pikipiki, 16, 17, 23, 42, 43, 66

Sheria ya Kusogea, 31

Kuendesha Gari Usiku, 13, 20, 73

Uchunguzi wa Mfumo wa Gari, 61

Maegesho ya Sambamba, 29

Wazazi, 21, 62, 73

Gari la Polisi, 31

Thibitisho la

Utambulisho, 16 Ya

muda, 15, 21, 73

Kivuko cha reli, 29, 32, 37, 59

Mahitaji ya Makazi, 10

Haki ya Njia, 28, 31, 32, 64

Mageuko ya Kulia, 31

Kuteleza , 48

Magari Yanayoenda Polepole 44

Taarifa za Usalama wa Jamii, 8, 9

Vikomo vya kasi, 34, 38

Kusimama, 25, 42, 56

Abiria Vijana, 73

Kutahiniwa 14

Treni, 33

Ishara ya Kugeuka, 26

Wanajeshi wa Marekani, 10

Uraia wa Marekani, 9

VERMONT

**Jimbo la Vermont**
*Mamlaka ya Usafiri*
IDARA YA MAGARI
120 State Street
Montpelier, Vermont 05603-0001
dmv.vermont.gov

Kwa: